JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2023

## URAIA NA MAADILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2023

# 06 URAIA NA MAADILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI ........ 2

2.1 Swali la 1. Kuwa Mwadilifu ........ 3

2.2 Swali la 2: Kuheshimu Jamii ........ 11

2.3 Swali la 3: Kuithamini Jamii ........ 20

2.4 Swali la 4: Kuwa Mwajibikaji ........ 27

2.5 Swali la 5: Kuithamini Jamii ........ 33

2.6 Swali la 6: Kudumisha Amani ........ 42

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ........ 53

4.0 HITIMISHO ........ 54

5.0 MAPENDEKEZO ........ 55

*Kiambatisho: Ulinganifu wa Ufaulu wa Wanafunzi kati ya Mwaka 2023 na 2022* ........ 57


**DIBAJI**

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2023 katika somo la Uraia na Maadili. Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya upimaji katika somo hili.

Ufaulu wa wanafunzi katika upimaji huu wa SFNA 2023 ni mzuri kwa sababu wanafunzi 1,321,137 (85.52%) walifaulu na wanafunzi 223,738 (14.48%) hawakufaulu. Taarifa inabainisha kuwa wanafunzi waliofaulu waliyaelewa maswali na walikuwa na uelewa wa kutosha katika aina mbalimbali za umahiri uliopimwa. Wanafunzi walioshindwa maswali (umahiri) kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022 inaonekana kuwa wanafunzi walikuwa na changamoto katika maeneo mbalimbali ukiwemo uelewa mdogo wa umahiri uliopimwa, kushindwa kubaini matakwa ya maswali, kushindwa kuhawilisha maarifa na kukosa ujuzi wa kujibu baadhi ya maswali kama vile; ufahamu, kuchunguza picha na maswali ya majibu mafupi.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa taarifa hii itawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa changamoto zilizowakabili wanafunzi katika kujibu maswali zinapatiwa ufumbuzi ili kuboresha ufaulu katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne.

Baraza linapenda kutoa shukrani za dhati kwa maafisa mitihani na wadau wengine wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) katika somo la Uraia na Maadili ulifanyika Oktoba 2023. Jumla ya wanafunzi 1,693,438 walisajiliwa kufanya upimaji huu ambapo wanafunzi 1,545,149 (92.24%) walifanya upimaji huu. Ufaulu wa wanafunzi katika somo hili unaonesha kuwa wanafunzi 1,321,137 (85.52%) walifaulu na wanafunzi 223,738 (14.48%) hawakufaulu. Ufaulu huu umeongezeka kwa asilimia 0.67 ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo wanafunzi 1,350,477 (84.85%) walifaulu upimaji huo.

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne somo la Uraia na Maadili mwaka 2023 ulikuwa na jumla ya maswali sita (6) yaliyogawanyika katika sehemu A na B yakiwa na vipengele 25. Sehemu A ilikuwa na maswali matatu (3) yenye vipengele 13 vyenye jumla ya alama 26. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yenye vipengele 12 vyenye jumla ya alama 24. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu A na B. Upimaji ulikuwa na jumla ya alama 50.

Katika sehemu A, swali la kwanza lilikuwa na vipengele vitano (i) – (v) vya kuchagua jibu sahihi ambapo wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku. Swali la pili lilikuwa na vipengele vinne vya kuoanisha na liliwataka wanafunzi kuoanisha maelezo kuhusu majukumu ya viongozi wa mtaa/kijiji katika Kifungu A na viongozi husika katika Kifungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano. Swali la tatu katika sehemu hii lilikuwa la kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Kila kipengele cha swali katika sehemu hii kilikuwa na uzito wa alama 2, hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 26.

Aidha, katika sehemu B, swali la Nne lilikuwa na vipengele vitano. Kipengele cha kwanza (a) kilitolewa kama mfano na hivyo

mwanafunzi alitakiwa kujibu vipengele vinne (b) – (e). Katika swali hili, wanafunzi walitakiwa kujibu kwa kuonesha matendo ya kuwa na nidhamu na kutokuwa na nidhamu kwa kuweka alama ya vema (√) kwenye tendo husika katika kisanduku. Katika swali la tano, wanafunzi walipewa picha ambayo walitakiwa kuichunguza na kisha kujibu maswali manne (4) waliyopewa. Swali la mwisho katika sehemu hii ni swali la sita (6) ambalo liliwataka wanafunzi kusoma kifungu cha habari kwa makini na kisha kuandika majibu katika sehemu zilizoachwa wazi.

Taarifa hii inachambua maswali yote sita yaliyotoka katika umahiri wa aina tano kati ya sita kama ulivyoainishwa katika muhtasari wa somo la Uraia na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la III - VII. Uchambuzi huu pia unabainisha idadi au asilimia ya wanafunzi walioweza au walioshindwa kuandika majibu sahihi na sababu zilizowafanya washindwe kuandika majibu hayo.

Viwango vya ufaulu wa jumla vimegawanywa katika makundi matatu ya ubora wa ufaulu kwa kuzingatia asilimia ya wanafunzi waliofaulu katika swali husika. Kiwango cha ufaulu cha asilimia 0 – 33 ya wanafunzi katika swali kinahesabika kuwa ni hafifu, 34 – 66 ni wastani na asilimia 67-100 ni kiwango kizuri. Viwango vya ufaulu vimewakilishwa na rangi tofauti: nyekundu (ufaulu hafifu), njano (ufaulu wa wastani) na kijani (ufaulu mzuri). Hivyo, ulinganifu wa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika kila umahiri na maswali katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022 umewasilishwa katika Kiambatisho.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI


Sehemu hii inachambua ufaulu wa wanafunzi katika kila swali kwa kuonesha jumla ya wanafunzi waliofanya swali husika na kuelezea ubora wa majibu yao. Pia, viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika kila swali vimewekwa katika makundi manne ambayo ni ufaulu mzuri sana, mzuri, wastani na dhaifu. Lengo ni

kuonesha kiwango cha utendaji cha wanafunzi katika swali husika kwa kuzingatia mgawanyo wa alama katika swali hilo.

## 2.1 Swali la 1: Kuwa Mwadilifu

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwadilifu*. Swali lilikuwa la kuchagua herufi ya jibu sahihi na lilikuwa na vipengele vitano (i) – (v) ambapo kila kimoja kilikuwa na alama 2. Wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo manne (A – D) yaliyowekwa kila baada ya shina la swali la kuchagua jibu sahihi kisha kuiandika herufi katika kisanduku kwenye karatasi ya upimaji.

Takwimu zinaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri kwa kuwa wanafunzi 1,262,385 (81.71%) waliofanya swali hili walipata alama 4 mpaka 10 kati ya alama 10 za swali hili. Hata hivyo, wanafunzi wengine 282,652 (18.29%) walikuwa na ufaulu hafifu kwani walipata alama 0 mpaka 2. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1.




**Chati Na. 1**: *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 1 umefanyika kama ifuatavyo:

(i) Ipi kati ya hizi ni wajibu wa mwanafunzi?
- A Kwenda shule na kupata elimu.
- B Kusoma kwa bidii na kupata chakula.
- C Kupata elimu na kuwasaidia wazazi.
- D Kwenda shule na kusoma kwa bidii.

Kipengele hiki cha swali kilihusu umahiri mahususi wa *Kusimamia haki*. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua maana ya dhana ya wajibu na haki za wanafunzi. Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha, walichagua jibu sahihi D, *Kwenda shule na kusoma kwa bidii*. Walikuwa wanafahamu kwamba wajibu unarejelea jambo au majukumu fulani ambayo mtu anatakiwa kutimiza. Unahusisha kuwajibika kwa matendo ya mtu na matokeo hutokana na matendo hayo. Aidha, wanafunzi walielewa kuwa haki ni stahili ambazo watu au mtu mmoja mmoja anazo katika jamii. Zinaweza kuwa za kisheria, maadili, au zitokanazo na kanuni za haki na usawa. Mifano mingine ya wajibu wa mwanafunzi ni kujitunza, kusimamia mambo yako, kuwa mwangalifu wa mazingira na kutimiza majukumu ya nyumbani na shuleni. Majukumu mengine ni pamoja na kutii sheria na kanuni za shule, kuwa na tabia ipasayo na kuonesha nidhamu binafsi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kuelewa dhana ya wajibu na haki, walichagua vipotoshi A, *Kwenda shule na kupata elimu*, B, *Kusoma kwa bidii na kupata chakula* na C, *Kupata elimu na kuwasaidia wazazi*. Hawakutambua kuwa vichaguzi hivyo vilikuwa kinyume na matakwa ya swali kwa sababu viliangazia wajibu na haki za wanafunzi kwa pamoja. Kwa mfano, kipotoshi A, *Kwenda shule na kupata elimu* kilihusu haki ya mtoto kupata elimu kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Elimu ya Tanzania namba 25 ya mwaka 1978 ambayo inaeleza kuwa elimu ya msingi ni ya

lazima kwa kila mtoto aliyefikisha umri wa miaka saba. Pia, kipotoshi B, *Kusoma kwa bidii na kupata chakula*, kiliangazia haki ya mtoto kula mlo kamili ambao ni muhimu kwa afya njema, ukuaji na maendeleo ya mtoto. Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi C, *Kupata elimu na kuwasaidia wazazi*, hawakutambua kwamba kupata elimu si wajibu bali ni haki ya mwanafunzi na kusaidia wazazi ni wajibu wa jumla ambao unaweza kufanywa na mwanafunzi yeyote anayewajibika katika familia. Kwa mfano, kusaidia kufanya kazi za nyumbani na kulisha mifugo.

(ii) Utawasilisha wapi taarifa kuhusu tendo la ukiukwaji wa haki za binadamu katika jamii yako?

A Mahakamani

B Kituo cha Polisi

C Bungeni

D Magereza

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *Kusimamia haki* na lilipima uelewa wa wanafunzi wa mamlaka zinazohusika kutetea ukiukwaji wa haki za binadamu katika jamii. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi B, *Kituo cha Polisi*, walikuwa na ufahamu wa kutosha kwamba kituo cha polisi ni ofisi ya utawala kwa ajili ya utekelezaji wa sheria ambapo maafisa wa polisi wanafanya kazi. Maafisa wa polisi wana jukumu la kudumisha utulivu na usalama wa umma, kuchunguza na kuzuia uhalifu na hutumika kama rasilimali ya jamii kwa usaidizi na ulinzi. Jeshi la Polisi limepewa mamlaka na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 9 ya mwaka 1985 kukamata, kupekua, kuzuia na kuchunguza utendaji wa makosa ya jinai na kufungua kesi za jinai katika mahakama. Kwa ufahamu huo, wanafunzi walifahamu kwamba kuvunja haki za binadamu ni kosa la jinai. Kwa hiyo, kituo cha polisi kilikuwa mahali pazuri pa kuripoti.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Mahakamani*, hawakujua kwamba mahakama ni chombo cha kiserikali kilichoidhinishwa kutatua migogoro ya

kisheria, kusimamia haki, na kutafsiri sheria. Mahakama ni mahali rasmi na hufanya kazi bila upendeleo kwa kusuluhisha mizozo, kuzingatia utawala wa sheria na kulinda haki za mtu binafsi, na kuweka vielelezo vya kisheria vinavyoongoza maamuzi ya siku zijazo. Wanafunzi wa aina hiyo walipuuza ukweli kwamba ukiukwaji wa haki za binadamu ni kosa la jinai ambalo haliwezi kuchunguzwa na mahakama badala yake, jeshi la polisi ni mamlaka iliyopewa kuchunguza na kuwafikisha wahalifu katika mahakama kwa taratibu zaidi za kisheria.

Kadhalika, wanafunzi waliochagua kipotoshi C, *Bungeni,* hawakufahamu ukweli kwamba bunge ni chombo kikuu cha kutunga sheria katika nchi, chenye jukumu la kusimamia serikali, na kuwakilisha maslahi ya umma. Bunge linahakikisha uwakilishi wa maoni na maslahi mbalimbali ya wananchi, kuwezesha upitishaji wa sheria na sera kupitia michakato ya kidemokrasia na kuiwajibisha serikali kupitia mijadala na usimamizi. Licha ya mamlaka ya Bunge kuunda kamati ya dharura kuchunguza tuhuma zozote za ukiukwaji wa haki za binadamu na kupendekeza njia ya utekelezaji kwa serikali, haliruhusiwi kisheria kukamata, kuzuia na kufungua kesi mahakamani.

Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Magereza*, hawakufahamu kuwa gereza ni kituo ambacho watu wanafungwa kama adhabu kwa kutenda uhalifu. Gereza hilo hutumika kama kizuizi kwa wakosaji watarajiwa, hulinda jamii kwa kuwatenga watu hatari na hutoa programu za urekebishaji ili kuwasaidia wahalifu kujumuika tena katika jamii. Wanafunzi waliochagua kipotoshi hiki walipaswa kuelewa kuwa gereza hilo lipo chini ya Jeshi la Magereza ambalo linapokea, kusimamia kwa karibu na kuwalinda wafungwa baada ya kutiwa hatiani na mahakama ili kutumikia adhabu kwa kosa walilofanya. Hivyo, si mahali sahihi pa kuripoti tuhuma za ukiukwaji wa haki za binadamu.

(iii) Kitendo cha kumuadhibu mtoto ambaye hajatenda kosa lolote kinaonesha nini?

A Kuwajibika kwa mzazi na mwalimu
B Kulinda haki ya mtoto
C Kuvunja haki za mtoto
D Kulinda makosa ya mtoto

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mahususi wa *Kusimamia Haki* na lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini matendo yanayolinda au yanayokiuka haki za watoto. Jibu sahihi lilikuwa chaguo C, *Kuvunja haki za mtoto*. Jibu hilo lilichaguliwa na wanafunzi ambao walikuwa na ufahamu juu ya ukiukwaji wa haki za watoto, walijua kwamba dhana hii inarejelea ukiukwaji au kutozingatiwa kwa haki na uhuru ambao ni stahiki ya watoto. Ukiukwaji wa haki za watoto unaweza kuwa wa aina nyingi kama vile, ubaguzi, mateso, mauaji ya kiholela, udhibiti, kazi za kulazimishwa, na kunyimwa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, elimu na huduma za afya. Kwa taarifa hizo wanafunzi walikuwa wanafahamu kuwa kumuadhibu mtoto asiye na hatia ni kitendo cha kumfanya mtoto ateseke au kuwajibika kwa kosa ambalo hakulifanya na kwa kufanya hivyo haki ya mtoto inadhulumiwa. Pia walijua umuhimu wa kusimamia njia bora na za ufanisi za kushughulikia au kurekebisha tabia isiyofaa ya mtoto kwa kuweka hatua za kinidhamu ambazo hazina madhara kwa mtoto kimwili na kisaikolojia. Hatua kama hizo ni pamoja na kuelewa chanzo cha tabia na kufuatilia mabadiliko yake. Pia walijua kuwa kuadhibu mtoto kwa kosa ambalo hakulifanya kunamuumiza mtoto asiye na hatia na kumfanya awe na wasiwasi na mfadhaiko na hivyo kunaweza kusababisha tabia isiyofaa katika siku zijazo.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Kuwajibika kwa mzazi na mwalimu* hawakujua kuwa mtoto asiye na hatia hastahili adhabu. Walishindwa kutambua kwamba adhabu inapaswa kutolewa kwa mwanafunzi asiye na

nidhamu na mwenye tabia mbaya kwa madhumuni ya kurekebisha tabia zake na si kwa mtoto asiye na hatia. Aidha, ni wajibu wa kila mwanajamii wakiwemo walimu, wazazi na hata serikali kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyovyote vinavyohatarisha ustawi wao.

Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Kulinda haki ya mtoto* walishindwa kutofautisha hatua za ukiukwaji na ulinzi wa haki za mtoto. Wanafunzi kama hao walipaswa kuelewa kwamba kulinda haki za mtoto kunahusisha utekelezaji wa hatua na miundo ya kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji, kutelekezwa, unyonyaji na ukatili unaoathiri mtoto. Kwa mantiki hiyo, wanafunzi walitarajiwa kutambua kuwa adhabu kwa mtoto asiye na hatia inaleta madhara zaidi kwa mtoto na kukiuka haki zake kuliko kumlinda.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Kulinda makosa ya mtoto,* pia hawakuwa sahihi kwa sababu kulinda makosa ya mtoto kunahusisha kuficha makosa ya mtoto ili yasifichuliwe au kuchukuliwa kuwa hayafai na watu wengine. Katika mtazamo huu, kulinda makosa ya mtoto kuna uwezekano wa kutetea na kumtia moyo mtoto kuendelea kufanya makosa yale yale, na hivyo, kumnyima mtoto nafasi ya kujifunza kutokana na makosa baada ya kuchukuliwa kwa makini hatua za kurekebisha tabia. Kwa kweli, kuruhusu watoto kujifunza kutokana na makosa yao husaidia katika kujenga ustahimilivu, kuongeza kujiamini na kuwaruhusu kukuza ujuzi muhimu wa kijamii na kihisia. Kwa kuzingatia maelezo haya, kulinda makosa ya mtoto hakuwezi kuoneshwa kwa kitendo cha kumwadhibu mtoto asiye na hatia. Badala yake, vitendo vyote viwili kwa njia moja au nyingine huathiri ustawi wa mtoto.

(iv) Unawajibika kufanya nini unapomwona mtu amedondosha fedha bila kujua?

A Kuokota fedha na kuzificha

B Kuokota fedha na kukimbia nazo

C Kuokota fedha na kumrudishia

D Kuokota fedha na kuzitumia haraka

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuaminiwa katika jamii*. Lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu dhana ya uadilifu wa maisha ya mwanafunzi. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi C, *Kuokota fedha na kumrudishia*, walijua kwamba uadilifu ni sifa ya kuwa mwaminifu, mkweli, na kuwa na kanuni thabiti za maadili ikiwa ni pamoja na kufanya jambo linalofaa, hata wakati hakuna mtu anayetazama. Inajumuisha uaminifu, uthabiti, uwajibikaji, na ujasiri katika kushikilia maadili.

Pia, walijua kwamba uaminifu hukua kwa kusema ukweli, kuwa mtiifu, kutimiza ahadi, kufichua maovu na kutunza mali ambayo mtu amepewa. Ujuzi huo wa kutosha uliwawezesha wanafunzi kubaini kuwa mtu mwaminifu ni mkweli, anaaminika, anafanya mambo yanayostahili na ni mtu mwenye tabia njema. Kwa hiyo, akiona fedha zimedondoshwa kwa bahati mbaya atazichukua na kuzirudisha kwa mmiliki.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wengine ambao hawakuwa na ujuzi wa kujenga tabia ya uaminifu walichagua majibu yasiyo sahihi A, *Kuokota fedha na kuzificha*, B, *Kuokota fedha na kukimbia nazo* D, *Kuokota fedha na kuzitumia haraka*. Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kwamba vichaguzi hivi vyote vilihusisha vitendo vinavyoonesha tabia ya kutokuwa na uaminifu. Kwa mfano, vitendo vya kuficha, kutumia na kukimbia na pesa huashiria nia ya kuchukua au kutumia kitu ambacho sio halali kwako, kwa hivyo ni tabia ya kutokuwa mwaminifu. Zaidi ya hayo, hawakujua kwamba mtu asiye mwaminifu, si mkweli, si mwenye kutegemewa, huficha vitu na nyakati fulani

hufanya maovu, huwaibia wengine, huwadanganya wengine na huwa hatimizi ahadi.

(v) Kitendo cha kumlazimisha mtoto kufanya kazi ngumu za mikono huonesha:
  A ukiukwaji wa haki za mtoto.
  B wajibu wa mtoto.
  C ukomavu wa mtoto.
  D nguvu alizonazo mtoto.

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mahususi wa *Kusimamia haki za watu wengine* na lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya vitendo vinavyokiuka haki za watoto. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi A, *ukiukwaji wa haki za mtoto*, walielewa kuwa utumikishwaji wa watoto ni kitendo cha kuwalazimisha kufanya kazi katika mazingira hatarishi, na kuwanyima haki zao za msingi. Ukiukwaji wa haki za watoto unamaanisha kunyimwa haki za kufurahia utoto kinyume cha sheria. Pia, wanafunzi waliochagua jibu hili walikuwa na ufahamu kwamba kazi ngumu ya mikono ni kazi ya kimwili ya binadamu ambayo inahusisha matumizi ya nguvu zaidi za mwili na misuli ili kuikamilisha. Ukweli huo ni kwamba kumfanyisha mtoto kazi ngumu ya mikono si tu kwamba ni hatari kiakili, kimwili, kijamii na kimaadili bali pia humnyima mtoto fursa ya kuhudhuria shule na mbaya zaidi, kunamnyima utoto wake, uwezo wake, heshima na inadhuru ukuaji wao wa kimwili na kiakili.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi B, *wajibu wa mtoto*. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha kati ya wajibu na haki za watoto. Hawakuelewa vizuri kwamba kumlazimisha mtoto kufanya kazi ngumu ya mikono si wajibu wa mtoto bali ni kinyume cha haki zake kwa sababu mtoto hajakomaa kiasi cha kufanya kazi nzito. Katika suala hili, wanafunzi walipaswa kujua kwamba mtoto kama mwanajamii ana majukumu fulani ya kutekeleza kulingana na

umri wake, kwa mfano, kufanya kazi kwa bidii, kusaidia wazazi katika baadhi ya kazi za nyumbani, kushiriki katika shughuli za maendeleo ya jamii na kulinda mazingira. Majukumu hayo humwandaa mtoto kuwa mwanajamii mwenye tija na anayewajibika kinyume na kumfanyisha kazi ya kulazimishwa ambayo inamweka mtoto katika unyonyaji, udhalilishaji na majanga ya kiafya.

Katika hali hiyo hiyo, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi C, *Ukomavu wa mtoto*. Hawa walishindwa kuelewa kwamba ukomavu wa mtoto ni uwezo wake kuitikia mazingira na kwa namna ifaayo. Kimsingi ni mchakato unaojidhibiti ambao kwa upande wake hurahisisha ukuaji katika akili ya kawaida na uwajibikaji wa mtoto. Ukomavu wa mtoto umeainishwa katika maeneo ya ukomavu wa kimwili, kihisia, kijamii, kiakili na kimaadili. Kwa hali hiyo, kitendo cha kumlazimisha mtoto kufanya kazi ngumu za mikono, hakiwezi kuwa dalili ya ukomavu wa mtoto kwa sababu watoto hukomaa kwa kasi yao wenyewe katika kila eneo la ukuaji na ukomavu. Pia, mtoto anaweza kukomaa katika eneo moja na wakati huo huo akawa hajakomaa katika eneo lingine. Kwa mfano, mtoto anaweza kukomaa kimwili lakini wakati huohuo hajakomaa kiakili.


Wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *nguvu alizonazo mtoto* hawakuelewa kuwa mtoto anaweza kuwa na nguvu kimwili lakini haitoshi kusimamia kazi ngumu za mikono ambazo mara nyingi zinahitaji utimamu wa mwili na akili. Pia, walipaswa kutambua kwamba mtoto hufanya kazi ngumu za mikono kinyume na matakwa yake, kwa hiyo, hakuna njia ambayo hatua hii inaweza kutumika kuonesha uwezo wa mtoto badala ya kuashiria ukiukwaji wa haki za mtoto.

## 2.2 Swali la 2: Kuheshimu Jamii

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na katika umahiri mahususi wa *Kuipenda Tanzania kwa*

*kuenzi tunu za nchi na asili yake*. Swali lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu majukumu ya viongozi katika ngazi ya vijiji au mitaa. Swali liliwataka wanafunzi kuoanisha majukumu ya viongozi wa mtaa/kijiji katika fungu A na viongozi husika kutoka katika fungu B na kisha kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano kwa kila kipengele.

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa kiwango hafifu kwa kuwa wanafunzi 313,816 (20.31%) pekee ndio waliofaulu. Wanafunzi 1,231,361 (79.69%) walipata ufaulu wa alama 0 hadi 2, 215,909 (13.97%) walipata alama 4, 64,166 (4.15%) walipata alama 6 na 33,741 (2.19%) walipata alama 8. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2.




**Chati Na. 2**: *Ufaulu wa Wanafunzi Katika Swali la 2*

Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuoanisha majukumu ya viongozi wa Mtaa/Kijiji katika **Fungu A** na viongozi husika kutoka katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Fungu A | | Herufi | | Fungu B |
|---|---|---|---|---|
| (i) | Husimamia shughuli zote kwenye Mtaa/Kijiji. | (   ) | A. | Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Mtaa/Kijiji. |
| (ii) | Huongoza vikao vya Mtaa/Kijiji. | (   ) | B. | Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji. |
| (iii) | Huunda Baraza la Mtaa/Kijiji. | (   ) | C. | Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji. |
| (iv) | Huteua Afisa Mtendaji wa Mtaa au Kijiji. | (   ) | D. | Kamati ya Ulinzi na Usalama. |
| | | | E. | Mkurugenzi wa Halmashauri. |
| | | | F. | Diwani wa Kata. |

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 2.

Kipengele cha (i) kilimtaka mwanafunzi kuoanisha cheo cha kiongozi wa Mtaa/Kijiji anayehusika na *kusimamia shughuli zote kwenye Mtaa/Kijiji.* Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha walichagua *C Afisa Mtendaji wa Mtaa/kijiji*. Wanafunzi hawa walifahamu vyema kuwa nafasi ya *Afisa huyo* inatangazwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, ambacho ni chombo kilichoundwa na Sheria ya Utumishi namba 8 ya mwaka 2002 na kufanyiwa marekebisho katika Sheria ya 2007 namba 18 kifungu cha 29 (1). Pia, Afisa Mtendaji wa mtaa/kijiji anawajibika kutunza kumbukumbu, utekelezaji wa sera na ushirikishwaji wa jamii.

Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Wenyeviti wa kamati mbalimbali za Mitaa/Vijiji* hawakuwa sahihi kwa sababu walipaswa kuelewa kwamba kamati za vijiji/mitaa zinawajibika kwa maendeleo ya jamii, utawala wa mitaa, kuhusika kusimamia

utoaji wa huduma za msingi za kijamii na zinahusika katika utatuzi wa migogoro katika serikali ya kijiji/mtaa.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi waliolinganisha na kipotoshi B, *Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji*, hawakufahamu kuwa ana wajibu wa kuwakilisha Mtaa/Kijiji katika mikutano ya Maendeleo ya Kata (WDC). Pia, anaitisha na kuongoza mikutano ya halmashauri ya kijiji na mikutano ya jumla ya kijiji/mtaa.

Zaidi ya hayo, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi D, *Kamati ya Ulinzi na Usalama*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa jukumu la kamati hii si kusimamia shughuli za Mtaa/Kijiji bali mara nyingi inahusika katika kudumisha ulinzi na usalama wa eneo hilo na kushirikiana na vyombo vya sheria ili kuhakikisha usalama wa jamii.

Aidha, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi E, *Mkurugenzi wa Halmashauri*. Wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa Mkurugenzi ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Halmashauri. Anahakikisha kuwa kazi na majukumu yote katika Halmashauri yanatekelezwa kwa mujibu wa sheria na maelekezo na mipango ya Baraza la madiwani, anapokea na kusikiliza matatizo, changamoto na malalamiko kutoka kwa wananchi katika halmashauri husika. Hivyo, si kweli kwamba mkurugenzi wa halmashauri anawajibika kusimamia shughuli zote katika ngazi ya mtaa/kijiji.

Mwisho, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi F, *Diwani wa Kata,* hawakugundua ukweli kwamba diwani ni kiongozi wa kisiasa ambaye anachaguliwa na wananchi katika kata husika, na anawawakilisha wananchi kwenye vikao vya Halmashauri ya Wilaya. Diwani anaongoza vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Kata. Diwani wa kata ni kama daraja linalounganisha watu ndani ya kata na Halmashauri ya Wilaya.

Katika kipengele (ii), wanafunzi walitakiwa kubainisha kiongozi anayeongoza vikao vya mtaa/kijiji kutoka kwenye Fungu B. Wanafunzi wenye ufahamu wa kutosha wa majukumu ya viongozi katika muundo wa serikali ya mtaa/kijiji walibaini jibu sahihi B*, Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji*. Wanafunzi hao walifahamu vyema kwamba Mwenyekiti wa mtaa/kijiji huchaguliwa na wakazi wa mtaa/kijiji kupitia taratibu rasmi za uchaguzi chini ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za mitaa. Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/Kijiji anasimamia miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa katika eneo lake la mamlaka. Aidha, mwenyekiti husimamia shughuli za amani na usalama za wananchi na mali zao katika kijiji/mtaa. Vilevile, husimamia usafi wa mtaa/kijiji na kuwawakilisha wananchi kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi A, *Wenyeviti wa kamati mbalimbali za mtaa/kijiji*. Hawakuzingatia ukweli kwamba, wenyeviti wanaratibu na kusimamia shughuli za kila siku za kamati wanazoziongoza. Kwa mtazamo huu, wenyeviti wa kamati za mtaa/kijiji hawajaidhinishwa kimuundo kuongoza mkutano wa mtaa/kijiji badala yake mamlaka hayo yanakabidhiwa kwa Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji.

Halikadhalika, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi C, *Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji*. Hawa hawakujua kuwa mgawanyo wa madaraka na mamlaka katika muundo wa Serikali ya mtaa/kijiji inamtambua Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji kama Katibu wa Mkutano Mkuu wa mtaa/kijiji na mikutano ya halmashauri. Walitakiwa kutambua kwamba aliyepewa mamlaka ya kuongoza mkutano wa Mtaa/Kijiji ni Mwenyekiti wa mtaa/kijiji.

Zaidi ya hayo, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi D, *Kamati ya Ulinzi na Usalama*. Hawakujua kwamba kamati za ulinzi na usalama hazina mamlaka ya kuongoza mkutano wa mtaa/kijiji badala yake jukumu lake kuu ni kudumisha amani na

utulivu katika mtaa/kijiji kwa kuhakikisha ufuataji wa sheria kwa wananchi wote wa mtaa/kijiji hicho.

Aidha, waliochagua kipotoshi E, *Mkurugenzi wa Halmashauri* hawakuelewa na elimu ya muundo wa serikali ya mtaa/kijiji. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya anapatikana katika ngazi ya Wilaya ya muundo wa serikali ya mitaa na si katika ngazi ya kijiji/mtaa. Yeye ndiye mtendaji mkuu wa halmashauri ya Wilaya na anasimamia utendaji wa halmashauri, anasimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya halmashauri na ana jukumu la kusimamia rasilimali fedha za halmashauri.

Mwisho, wanafunzi waliochagua kipotoshi F, *Diwani wa Kata* hawakuwa sahihi kwa kuwa Diwani huyo anaweza kualikwa kuhudhuria mkutano wa mtaa/kijiji lakini Sheria ya mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inayoanzisha serikali za mitaa haitoi mamlaka kwa diwani huyo kuwa mwenyekiti wa mikutano ya mtaa/kijiji badala yake imeweka mamlaka hayo kwa mwenyekiti wa mtaa/kijiji. Sheria hiyo hiyo inaweka bayana kuwa Diwani wa Kata anawajibika kupeleka mbele ya Baraza madai ya wananchi wake katika Kata, husimamia miradi ya maendeleo ya kata na hufanya maamuzi kwa niaba ya wananchi wake katika halmashauri.

Kipengele cha (iii) kiliwataka wanafunzi kubaini wajumbe wanaounda Baraza la mtaa/kijiji kutoka kwenye Fungu B. Wanafunzi wenye uelewa juu ya muundo wa serikali ya mtaa/kijiji walibaini jibu sahihi A, *Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Mitaa/Vijiji*. Hawa walikuwa wanafahamu kuwa Wenyeviti wa kamati za Mtaa/Vijiji ni wajumbe wa halmashauri ya mtaa/kijiji ambao wanasimamia kamati mbalimbali za halmashauri ya mtaa/kijiji. Kazi yao kuu ni kusimamia na kuratibu shughuli za kila siku za kamati zao na wanachaguliwa miongoni mwa wajumbe wa baraza.

Hata hivyo, kwa kutojua baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi B, *Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji*. Hawakujua kuwa Mwenyekiti wa mtaa/kijiji anawajibika kuandaa daftari la wakazi na kutunza taarifa nyingine zinazohusiana na maendeleo ya kijiji/mtaa. Pia, anaongoza vyombo viwili vikubwa vya maamuzi vya mtaa/kijiji ambavyo ni Mkutano wa mtaa/kijiji na Halmashauri ya mtaa/kijiji. Aidha, anawajibika kutatua migogoro midogo midogo inayotokea kwenye ngazi ya kijiji/mtaa, na kusimamia masuala ya afya katika eneo la mamlaka yake pamoja na utekelezaji wa kampeni za afya dhidi ya magonjwa ya kuambukiza ikiwemo UKIMWI/VVU.

Vilevile, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi C, *Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji.* Wanafunzi hao hawakufahamu kuwa Afisa Mtendaji wa mtaa/kijiji ndiye katibu wa Baraza la Mtaa/Kijiji na ni Afisa mwenye dhamana ya kusimamia kila shughuli za mtaa/kijiji ikiwa ni pamoja na kutekeleza sera na maamuzi yanayotolewa na ngazi za juu za serikali za mitaa na kutunza kumbukumbu zinazohusiana na kijiji au mtaa, ikiwa ni pamoja na takwimu za idadi ya watu, matumizi ya ardhi na shughuli za kifedha zinazohusiana na serikali za mitaa.

Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Kamati ya Ulinzi na Usalama* walishindwa kuelewa kuwa kamati ya ulinzi na usalama inaundwa na Baraza la mtaa/kijiji na ni chombo cha utendaji ambacho kinafanya kazi kupitia kamati mbalimbali mojawapo ikiwa ni kamati ya ulinzi na usalama. Pia, kamati inaratibu shughuli za kukabiliana na dharura ndani ya kijiji/mtaa na wakati fulani, zinaweza kushiriki katika shughuli za polisi jamii. Kwa hiyo, chaguo hili halikuweza kuendana na usahihi wa hitaji la swali hili.

Vilevile, wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi E, *Mkurugenzi wa halmashauri*. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha viongozi katika muundo wa serikali ya mtaa/kijiji na ule wa

halmashauri ya wilaya. Walishindwa kutambua kuwa mkurugenzi wa halmashauri hufanya ufuatiliaji na kutathmini matokeo ya miradi na programu za halmashauri.

Aidha, wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi F, *Diwani wa Kata,* hawakuelewa kwamba, Diwani wa kata ni mwakilishi wa wananchi katika mikutano yote ya kata katika wilaya hiyo, ni mwenyekiti wa mikutano mbalimbali inayofanyika katika kata na hushirikiana na maafisa watendaji katika Kata kuendesha miradi na shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba, diwani ni miongoni mwa wajumbe wanaounda halmashauri ya mtaa au kijiji ingawa ni mjumbe wa Baraza kamili la wilaya/manispaa husika.

Kipengele cha (iv) kiliwataka wanafunzi kutambua afisa ambaye huteua afisa mtendaji wa mtaa au kijiji kutoka katika Fungu B. Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha kuhusu majukumu ya watumishi ndani ya halmashauri walichagua jibu sahihi E, *Mkurugenzi wa Wilaya*. Hawa walifahamu kuwa Mkurugenzi wa Wilaya hupata kibali cha kupata/kuajili watumishi wa aina hiyo ya maafisa watendaji. Vilevile, walijua kuwa Mkurugenzi wa halmashauri ni msimamizi wa watumishi wa umma wa halmashauri, hukuza uchumi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na huhakikisha uwepo wa uwajibikaji na utawala bora katika halmashauri.

Zaidi ya hayo, wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Wenyeviti wa* mtaa/kijiji *mbalimbali*, hawakutambua kuwa wenyeviti wa kamati za mitaa/vijiji wanashirikiana bega kwa bega na viongozi wengine wa Serikali ya mtaa/kijiji ili kuhakikisha uratibu na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii, upatikanaji wa huduma za kijamii kama maji, elimu, huduma za afya na miundombinu mingine.

Hali kadhalika, wanafunzi wengine ambao hawakuwa na ufahamu wa majukumu ya viongozi wa mtaa/kijiji walichagua kipotoshi B, *Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji*. Walishindwa kuelewa kuwa Mwenyekiti wa mtaa/kijiji ni kiongozi wa kisiasa na hajapewa mamlaka ya kuajiri watumishi wa umma. Pia, hawakufahamu kuwa Afisa Mtendaji wa mtaa/kijiji ni mtumishi wa umma anayeshirikiana na Mwenyekiti katika kutekeleza majukumu yake hususan ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Zaidi ya hayo, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi C, Afisa Mtendaji wa mtaa/kijiji. Huyu ana wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sheria za serikali ya mtaa/kijiji, kushirikiana na mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji kuleta maendeleo ya wananchi na kukusanya mapato ya serikali ya mtaa/kijiji. Ni kweli Afisa Mtendaji wa mtaa/kijiji ni mwajiriwa anayeweza kuhamishwa kutoka eneo moja kwenda jingine.


Aidha, wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi D, *Kamati ya Ulinzi na Usalama* hawakufahamu kuwa kamati ina jukumu la kusimamia hali ya amani na usalama na kuhakikisha kuwa kuna mfumo mzuri wa kutoa taarifa za uhalifu wa aina mbalimbali katika eneo husika. Aidha, kamati hii inahusika katika kudumisha usalama wa ndani, kuratibu shughuli za kukabiliana na dharura ndani ya mtaa/kijiji, kushirikiana na vyombo vya kisheria ili kuhakikisha usalama na amani katika jamii, na katika baadhi ya matukio hushiriki katika shughuli za polisi jamii.

Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi F, *Diwani wa Kata*. walishindwa kutambua kuwa diwani anayo haki ya kutekeleza majukumu yake kama vile kuwawakilisha wananchi katika kikao kamili cha baraza la madiwani, kufuatilia utekelezaji wa miradi, na mipango mbalimbali ya maendeleo katika kata, ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali katika Kata, na kuelimisha wananchi mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya kiuchumi na

kijamii. Mwisho husaidia kutatua migogoro katika kata na kutoa mrejesho kwa wananchi juu ya hatua zilizochukuliwa.

### 2.3 Swali la 3: Kuithamini Jamii

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini Jamii.* Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi lililopo katika mabano na kuliandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri, kwani wanafunzi 1,071,513 (69.35%) waliofanya swali hili walifaulu kwa kupata alama 4 hadi 8. Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 279,294 (18.08%) walipata alama 4, wanafunzi 383,999 (24.85%) walipata alama 6 na wanafunzi 408,220 (26.42%) walipata alama 8. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 473,636 (30.65%) walikuwa na ufaulu hafifu wa alama 0 hadi 2. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 3**: *Ufaulu wa Wanafunzi Katika Swali la 3*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 3.

(a) Kufanya usafi wa mazingira ya shule ni jukumu la ________________________________________.
(viongozi wa shule, wanafunzi wote, kiranja wa shule)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kutunza mazingira*. Swali hili lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu jukumu lao katika shughuli za uhifadhi wa mazingira. Jibu sahihi lilikuwa ni *wanafunzi wote*. Jibu hili lilibainishwa na wanafunzi ambao walifahamu umuhimu wa kila mwanafunzi kushiriki katika kutunza mazingira ya shule. Walikuwa na ufahamu kuwa mazingira ya shule yanajumuisha mchanganyiko wa vifaa vyote vinavyopatikana shuleni ikiwa ni pamoja na majengo, bustani za maua, miti, viwanja vya michezo, vyanzo vya maji. Vilevile, walijua kuwa mazingira nadhifu huwavutia wanafunzi kupenda shule ambayo nayo hurahisisha mchakato mzuri wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa umuhimu huo, kila mwanafunzi anawajibika kuhifadhi mazingira ya shule kwa kuepuka utupaji taka usiofaa.

Kinyume chake, baadhi ya wanafunzi walichagua majibu yasiyo sahihi walitaja *viongozi wa shule*. Hawakujua kwamba hawa ni watu wenye nafasi za juu za utawala ndani ya shule, kama vile Mwalimu Mkuu, Mwalimu Mkuu Msaidizi na wafanyakazi wengine wakuu. Viongozi wa shule wanawajibika kwa usimamizi wa shule kwa ujumla na wao huweka maono na mwelekeo wa shule, hufanya maamuzi muhimu ya sera, husimamia programu za kitaaluma na za ziada, na kuhakikisha mazingira mazuri ya kujifunzia.

Zaidi ya hayo, wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi cha *kiranja wa shule* hawakuwa na ufahamu wa majukumu ya viranja shuleni. Walitakiwa kuelewa kwamba viranja wa shule ni wanafunzi walioteuliwa/kuchaguliwa kusaidia katika utawala na

nidhamu ya shule. Kawaida huchaguliwa kulingana na sifa zao za uongozi, uwajibikaji na tabia nzuri. Viranja wa shule husaidia kudumisha nidhamu, kuhakikisha kuwa sheria za shule zinafuatwa, na kusaidia kupanga matukio ya shule. Wanaweza pia kutumika kama kiunganishi kati ya wanafunzi na walimu na husaidia kushughulikia masuala ndani ya jumuiya ya shule.

(b) Moja kati ya rasilimali inayochangia kunyesha kwa mvua ni ___________________________________________.
(ardhi, majengo, msitu)

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri *mahususi wa Kutunza Mazingira*. Wanafunzi walitakiwa kutathmini nafasi ya misitu/miti katika kuhifadhi mazingira. Jibu sahihi lilikuwa *msitu*. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya uhifadhi wa mazingira. Walijua kwamba uhifadhi wa mazingira ni utaratibu wa kutunza ulimwengu na vilivyomo kwa uasili wake ili kuuzuia usiporomoke/usidunishwe. Walifahamu mchango wa rasilimali ya misitu katika usimamizi wa mzunguko wa maji, uhifadhi wa viumbe hai, udhibiti wa hali ya hewa, uzalishaji wa oksijeni, faida za kiuchumi, thamani ya kitamaduni na burudani, rasilimali za dawa, rutuba ya udongo, uzuiaji wa majanga ya asili, na utulivu wa hali ya hewa duniani.

Kinyume chake, wanafunzi, ambao walishindwa kuelewa dhana ya uhifadhi wa mazingira, walichagua *ardhi*. Hawa hawakujua kwamba inahusu sehemu ngumu ya uso wa dunia ambao haujafunikwa kabisa na maji. Inajumuisha kila kitu kilicho juu au kinachounganishwa na ardhi kama vile majengo, miti na maliasili. Ardhi ni rasilimali muhimu yenye umuhimu wa kiuchumi, kijamii na kimazingira. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kwamba ardhi si sehemu moja kwa moja katika mchakato wa kutengeneza mvua ingawa kwa njia moja au nyingine ardhi tupu inaweza kusababisha uvukizi usio na

uwiano unaosababishwa na joto jingi na kwa upande mwingine huweza kuzuia uundaji wa mvua.

Vilevile, wanafunzi waliochagua *majengo*, hawa hawakujua kuwa linarejelea muundo wenye paa na kuta ambazo kwa kawaida hujengwa kwa ajili ya watu kuishi, kufanya kazi au kushiriki katika shughuli mbalimbali. Majengo hutumka kwa madhumuni kadhaa na huchangia maendeleo ya jumla ya jamii. Majengo hutoa makazi, maeneo ya kazi nafasi za jamii kujiburudisha, na thamani ya usanifu na kitamaduni. Kwa hiyo, hayachangii kuleta mvua.

(c) Kiongozi wa wanafunzi mwenye jukumu la jumla la kusimamia usafi wa shule ni?

_______________________________________________.

(kiranja mkuu, kiranja wa darasa, kiranja wa michezo)

Kipengele hiki kilitungwa kutoka katika umahiri mahususi wa *Kutunza mazingira* kiliwataka wanafunzi kutambua cheo cha mtu mwenye jukumu la kusimamia usafi shuleni. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *kiranja mkuu*, walifahamu vyema kuwa ndiye kiongozi mkuu katika uongozi wa serikali ya wanafunzi shuleni. Kiranja mkuu ndiye msimamizi wa jumla wa viranja wengine. Kwa hiyo, Kiranja Mkuu wa shule ni mwakilishi wa wanafunzi kwenye utawala wa shule, husaidia katika nidhamu na ufuataji wa taratibu, hupanga na kuongoza matukio, huhimiza ubora wa kitaaluma, husaidia katika kutatua migogoro na kuimarisha ubora wa shule, na husimamia majukumu ya viranja wote katika kutekeleza majukumu yao. Kiranja mkuu wa shule, anachukua uwajibikaji wa jumla katika kusimamia usafi ili kuweka mazingira ya shule katika hali ya usafi na ya kuvutia kila wakati. Katika kufanya hivyo, anashirikiana na kiranja wa mazingira na walimu kuhakikisha kuwa zana za usafi zinapatikana na mipango ya kuhifadhi mazingira ya shule inafanyika kwa ufanisi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao hawakuwa na ufahamu wa kutosha wa majukumu ya usimamizi walichagua *kiranja wa darasa*. Hawa hawakuweza kubaini kuwa kiranja wa darasa ni mwanafunzi aliyechaguliwa kuwakilisha darasa. Ana jukumu la kudumisha utaratibu na nidhamu ndani ya darasa. Kiranja wa darasa, mara nyingi, huwasaidia walimu katika kazi mbalimbali; husaidia kudumisha hali ya utulivu darasani na hutumika kama mfano ya kuigwa kwa wanafunzi wenzake. Anaweza pia kupokea au kutoa taarifa muhimu kuhusu walimu na wanafunzi. Wanafunzi waliochagua jibu hili hawakujua ukweli kwamba mgawanyo wa majukumu katika muundo wa uongozi wa wanafunzi umempa mamlaka ya kiranja wa darasa kufanya kazi za ndani ya darasa.

Vilevile, wanafunzi waliochagua *kiranja wa michezo* hawakujua kuwa yeye ni msimamizi wa michezo anateuliwa kusimamia michezo na mazoezi ya kimwili shuleni na ndiye anayesimamia shughuli zote zinazohusiana na michezo shuleni. Kiongozi wa michezo kwa kawaida huwa na jukumu la kupanga na kuratibu matukio ya michezo, kuhimiza ushiriki katika mazoezi ya kimwili na kuhimiza maisha yenye afya na uchangamfu miongoni mwa wanafunzi. Anaweza kufanya kazi kwa karibu na walimu na makocha ili kuhakikisha kunakuwa na utendakazi mzuri wa programu za michezo. Kwa maelezo hayo, ni ukweli kwamba majukumu ya kiranja wa michezo yanahusu masuala yanayohusiana na michezo pekee. Hivyo, yeye hachukui jukumu la jumla la usafi wa shule kinyume na kiranja mkuu.

(d) Unapofanya kosa unaweza kusahihishwa na ________________________________________.
(Wazazi tu, mtu yeyote, walimu tu)

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mahususi wa *Kujijali na kuwajali wengine*. Liliwataka wanafunzi kutambua mtu anayewajibika kurekebisha makosa yanapofanywa na watu

wengine. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha walichagua jibu sahihi *mtu yeyote*. Hawa walijua kwamba kuwajali wengine sio tu kunasaidia na kutanguliza mahitaji ya wengine kabla ya masilahi yetu ya kibinafsi, lakini pia ni uwezo wa kusikia, kuelewa na kutambua mahitaji na hisia za wengine. Ustadi huu ni wa manufaa kwa vile unasisitiza watu kuwa na hisia ya kuwa na wajibu wa kimaadili, kufanya jitihada za uaminifu, kuingilia kati makosa ya wengine ili wawe salama. Hoja hii inadai kuwa kila mwanajamii anawajibika kimaadili kuwarekebisha wengine pale wanapofanya makosa ili warekebike kabla ya kufanya mambo ya kutisha. Kielelezo Na.1.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi kwa swali la 3.

3. Jibu vipengele (a) – (d) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(a) Kufanya usafi wa mazingira ya shule ni jukumu la Wanafunzi wote. (viongozi wa shule, wanafunzi wote, kiranja wa shule)

(b) Moja kati ya rasilimali inayochangia kunyesha kwa mvua ni msitu. (ardhi, majengo, msitu)

(c) Kiongozi wa wanafunzi mwenye jukumu la jumla la kusimamia usafi wa shule ni kiranja mkuu. (kiranja mkuu, kiranja wa darasa, kiranja wa michezo)

(d) Unapofanya kosa unaweza kusahihishwa na Mtu yeyote. (wazazi tu, mtu yeyote, walimu tu)

**Kielelezo Na.1.1**: *Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 3*

Kinyume chake, wanafunzi waliochagua *wazazi na walimu tu*, hawakujua kuwa ni wajibu wa kimaadili wa kila mwanajamii

kuchangia katika juhudi za pamoja za kujenga jamii yenye upendo na kujali. Walipaswa kufahamu kwamba licha ya jukumu la msingi ambalo wazazi na walimu wanalo katika kurekebisha makosa ya wanafunzi nyumbani na shuleni, wajibu huo haubaki kwao tu. Kwa mfano, kuwarekebisha watoto wanapofanya makosa huwasaidia kutambua makosa yao na kurekebisha tabia zao ipasavyo. Vilevile, inawasaidia kufanya uamuzi unaofaa, kuepuka tabia hatarishi, na kuzingatia malengo yao ya shule na maisha na kupata amani ya moyo kwa sababu wanahisi kupendwa na kujaliwa.

Katika muktadha wa Kitanzania, jukumu la kurekebisha makosa ya watoto kwa kawaida ni la mtu mmoja mmoja na taasisi mbalimbali zikiwemo; wazazi na familia, walimu na shule, jumuiya na wazee, serikali na sera na taasisi za kidini na kitamaduni. Kielelezo Na.1.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mwanafunzi katika swali la 3.

3. Jibu vipengele (a) – (d) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(a) Kufanya usafi wa mazingira ya shule ni jukumu la *waShule*. (viongozi wa shule, wanafunzi wote, kiranja wa shule)

(b) Moja kati ya rasilimali inayochangia kunyesha kwa mvua ni *ardhi*. (ardhi, majengo, msitu)

(c) Kiongozi wa wanafunzi mwenye jukumu la jumla la kusimamia usafi wa shule ni *kuSimamia uSafi Mazing.* (kiranja mkuu, kiranja wa darasa, kiranja wa michezo)


(d) Unapofanya kosa unaweza kusahihishwa na *wazazi*. (wazazi tu, mtu yeyote, walimu tu)

**Kielelezo Na.1.2**: Sampuli ya Majibu ya Mwanafunzi yasiyo sahihi katika Swali la 3

## 2.4 Swali la 4: Kuwa Mwajibikaji

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na umahiri mahususi wa *Kuwa na nidhamu binafsi*. Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini matendo yanayoakisi kuwa au kutokuwa na nidhamu. Swali lilikuwa na vipengele vitano (a) – (e) ambapo wanafunzi walitakiwa kubainisha kwa kuweka alama ya vema (√) kwenye matendo yanayoonesha kuwa na nidhamu au kutokuwa na nidhamu kwenye sehemu ya tendo husika katika kisanduku. Kipengele (a) kilitolewa kama mfano hivyo, mwanafunzi alitakiwa kujibu vipengele vinne (b) – (e).

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa kama ifuatavyo: wanafunzi 397,578 (25.73%) walipata alama 0 hadi 2; wanafunzi 216,065 (13.98%) walipata alama 4, wanafunzi 130,414 (8.44%) walipata alama 6, na wanafunzi 801,092 (51.85%) walipata alama 8. Ufaulu wa jumla kwa swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri kwa kuwa wanafunzi 1,147,571 (74.27%) walipata alama kuanzia 4 hadi alama 8 na wanafunzi 397,578 (25.73%) walipata alama 0 hadi alama 2. Hivyo hawakufanya vizuri. Chati Na 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.




**Chati Na. 4**: *Ufaulu wa Wanafunzi Katika Swali la 4*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 4. Swali liliulizwa kama ifuatavyo:

Jibu vipengele (b) – (e) kwa kuonesha matendo yanayoonesha Kuwa na nidhamu au kutokuwa na nidhamu kwa kuweka alama ya (√) kwenye sehemu inayohusika. Kipengele (a) kimetolewa **kama mfano**.

| **Kitendo** | **Kuwa na Nidhamu** | **Kutokuwa na Nidhamu** |
|---|---|---|
| (a) Kitendo cha mwanafunzi kuruka ukuta wa shule ili asiadhibiwe baada ya kuchelewa kufika shuleni. | | √ |
| (b) Kitendo cha mwanafunzi kutoka darasani muda wa vipindi na kufuata gari la matangazo. | | |
| (c) Kitendo cha mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote kwenye ratiba. | | |
| (d) Kitendo cha mtoto kupiga mswaki na kuoga kila siku. | | |
| (e) Kitendo cha mwanafunzi kuwahi shuleni akiwa hajavaa sare yenye nembo ya shule. | | |

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulionesha kuwa wanafunzi wenye maarifa ya kutosha ya kuwa na nidhamu, waliweza kutofautisha vitendo vinavyoonesha kuwa na nidhamu binafsi na kutokuwa na nidhamu binafsi. Walifahamu kuwa na nidhamu kuna maana ya kuwa na uwezo wa kudhibiti tabia, hisia na vitendo vya mtu mwenyewe. Inahusisha kufanya uchaguzi unaolingana na malengo na maadili ya muda mrefu

hata katika kukabiliana na changamoto au kuingiliwa. Nidhamu binafsi inayooneshwa na uwezo wa kudhibiti mawazo, hisia au tabia ya mtu. Katika mtazamo huu, mtu mwenye nidhamu binafsi ana uwezo wa kujitawala, kuwa na utashi, kuwa na subira na kuwa na uwezo wa kuamua vizuri.

Katika mazingira ya shule, wanafunzi walio na nidhamu wanatarajiwa kufanya na kukamilisha kazi kwa wakati, kuja shuleni mapema, kusoma kwa bidii na kufanya kazi bila uangalizi au bila usimamizi, kutii sheria za shule na kufuata ratiba, na kufanya usafi binafsi. Kwa mtazamo huo, wanafunzi waliofaulu kwa kuweka tiki (√) chini ya safu wima ya Kuwa na Nidhamu katika kipengele (c) na kipengele *Kitendo cha mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote kwenye ratiba* na kipengele (d) *Kitendo cha mtoto kupiga mswaki na kuoga kila siku*, walifahamu kuwa mwanafunzi mwenye nidhamu amedhamiria, ana subira na ana utashi, hivyo anakaa darasani na kubaki makini na masomo yake ili kufikia matarajio yake ya kitaaluma. Pia, mwanafunzi mwenye nidhamu anajali afya yake kwa kupiga mswaki na kuoga kila siku. Vilevile, walijua kwamba mbali na kuheshimu ratiba ya shule ya jumla, mwanafunzi mwenye nidhamu hutayarisha ratiba yake na kuifuatilia kwa ukaribu. Kwa hiyo, anajua anapotakiwa kuwa, kwa muda gani na kwa madhumuni gani.

Zaidi ya hayo, uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi wengine waliweza kuonesha vitendo vilivyoashiria kutokuwa na nidhamu kwa kuweka alama kwenye kipengele (b) *Kitendo cha wanafunzi kutoka nje ya darasa wakati wa saa za darasa na kulifuata gari la matangazo* na kipengele (e) *Kitendo cha mwanafunzi kuwahi shuleni akiwa hajavaa sare yenye nembo ya shule*. Wanafunzi hao walielewa kuwa matendo yote mawili yanadhihirisha kutokuwa na nidhamu. Wanafunzi hawa walifahamu kuwa ukosefu wa nidhamu unadhihirishwa na kutojizuia kufanya makosa, kutoamua vizuri, kuwa tegemezi, kutojipanga, kutowajibika na kutokuwa na maamuzi sahihi.

Waliona kwamba kwenda nje ya darasa muda wa masomo kunaonesha wanafunzi kutokuwa na mpangilio na ukosefu wa uamuzi sahihi. Kutokuwa na mpangilio kunachangiwa na kutokuwa na ratiba binafsi ya kuongoza shughuli za kila siku ilihali kutobainishwa kunadhoofisha uwezo wa mtu wa kuwa makini katika kufikia malengo yake. Ukosefu wa nidhamu miongoni mwa wanafunzi huwafanya kuwa tegemezi, kutowajibika na kutokuwa na maamuzi. Kwa hiyo, kunafanya wawe katika hatari ya kupata kwa urahisi majaribu.

Wanafunzi walioweka alama kwenye kipengele (b) na (e) walikuwa wanajua kuwa mwanafunzi mwenye nidhamu anatarajiwa kufuata sheria na kanuni za shule, kwa mfano kuvaa sare nzuri na safi za shule. Kushindwa kufuata sheria za shule kunaonesha utovu wa nidhamu, uzembe, makosa ya wazi na kutokuwa na heshima. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 4.

4. Jibu vipengele (b) – (e) kwa kuonesha matendo yanayoonesha **kuwa na nidhamu** au **kutokuwa na nidhamu** kwa kuweka alama ya (√) kwenye sehemu inayohusika. Kipengele (a) kimetolewa **kama mfano**.

| Kitendo | Kuwa na Nidhamu | Kutokuwa na Nidhamu |
|---|---|---|
| (a) Kitendo cha mwanafunzi kuruka ukuta wa shule ili asiadhibiwe baada ya kuchelewa kufika shuleni. | | √ |
| (b) Kitendo cha mwanafunzi kutoka darasani muda wa vipindi na kufuata gari la matangazo. | | √ |
| (c) Kitendo cha mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote kwenye ratiba. | √ | |
| (d) Kitendo cha mtoto kupiga mswaki na kuoga kila siku. | √ | |
| (e) Kitendo cha mwanafunzi kuwahi shuleni akiwa hajavaa sare yenye nembo ya shule. | | √ |

**Kielelezo Na.2.1**: *Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi Katika Swali la 4*

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kwamba kulikuwa na wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa ya kuwa na nidhamu kiasi kwamba walishindwa kutofautisha vitendo vinavyoonesha kuwa na nidhamu binafsi na vile vinavyoonesha kutokuwa na nidhamu. Hivyo, waliweka tiki (√) dhidi ya taarifa zisizo sahihi. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliweka tiki (√) kwenye kisanduku chini ya safu wima ya Kutokuwa na Nidhamu binafsi lakini kauli katika kipengele (c) *Kitendo cha mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote kwenye ratiba*, kilikuwa ni kitendo cha kujituma hivyo ishara ya kuwa na nidhamu. Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kwamba vitendo vya kufuata ratiba ya shule na kuhudhuria masomo ni ishara ya kujitolea na kuwa makini na kujiamulia mambo ambayo kwa hakika ni sifa za mtu kuwa na nidhamu.

Vilevile, baadhi ya wanafunzi walikosea (d) *Kitendo cha mtoto kupiga mswaki na kuoga kila siku* kama kitendo kinachoonesha kutokuwa na nidhamu. Wanafunzi hawa wangeweza kufahamu kuwa vitendo vya kupiga mswaki na kuoga kila siku vinaonesha tabia ya kujijali na kujipenda. Mtu anayejipenda na kujijali anajali afya yake vizuri, anaepuka kufanya mambo mabaya na ana tabia nzuri. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kwamba vitendo hivi vinahusika zaidi na kudumisha nidhamu kuliko kuonesha ukosefu wa nidhamu.

Hali kadhalika, kulikuwa na wanafunzi walioweka tiki (√) ikionyesha kitendo cha kuwa na nidhamu katika kipengele (b) *Kitendo cha mwanafunzi kutoka darasani muda wa vipindi na kufuata gari la matangazo*. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kwamba kitendo cha mwanafunzi kuondoka darasani na kufuata gari la matangazo hakioneshi kuwa na nidhamu. Badala yake, kinaonesha kuwa mwanafunzi haheshimu ratiba ya shule na hajadhamiria kupata masomo kwa vile haelekezi fikira darasani badala yake anaendelea kuzurura kwa hiyo, anaonesha tabia ya utovu wa nidhamu.

Zaidi ya hayo, wanafunzi wengine waliweka tiki (√) katika safu ya kuwa na nidhamu katika kipengele (e) *Kitendo cha mwanafunzi kuwahi shuleni akiwa hajavaa sare yenye nembo ya shule.* Wanafunzi hawa walikosa ufahamu kwamba kitendo cha kuja shuleni na sare zisizofaa kilichofanywa na mwanafunzi kilikuwa ni kutoheshimu walimu, wanafunzi wenzao na sheria za shule na hivyo, kilipaswa kuchukuliwa kama utovu wa nidhamu. Walitakiwa kuelewa kwamba mwanafunzi mwenye nidhamu atafuata kanuni na maadili ya shule kila wakati na kuonesha heshima kwa kila mtu. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa swali la 4.

4. Jibu vipengele (b) – (e) kwa kuonesha matendo yanayoonesha **kuwa na nidhamu** au **kutokuwa na nidhamu** kwa kuweka alama ya (√) kwenye sehemu inayohusika. Kipengele (a) kimetolewa **kama mfano.**


| **Kitendo** | **Kuwa na Nidhamu** | **Kutokuwa na Nidhamu** |
|---|---|---|
| (a) Kitendo cha mwanafunzi kuruka ukuta wa shule ili asiadhibiwe baada ya kuchelewa kufika shuleni. | √ | √ |
| (b) Kitendo cha mwanafunzi kutoka darasani muda wa vipindi na kufuata gari la matangazo. | √ | √ |
| (c) Kitendo cha mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote kwenye ratiba. | √ | √ |
| (d) Kitendo cha mtoto kupiga mswaki na kuoga kila siku. | | √ |
| (e) Kitendo cha mwanafunzi kuwahi shuleni akiwa hajavaa sare yenye nembo ya shule. | √ | |

**Kielelezo Na.2.2**: *Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 4*

## 2.5 Swali la 5: Kuithamini Jamii

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini Jamii* na umahiri mahususi wa *Kujijali na kuwajali wengine*. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi wa kubainisha matendo au tabia zinazoonesha kuwajali watu wengine. Katika swali hili, wanafunzi walipewa picha ambayo walitakiwa kuichunguza kwa makini kisha kujibu maswali kwenye vipengele (a) – (d).


Takwimu za ufaulu wa wanafunzi zinaonesha kuwa wanafunzi 871,137 (56.38%) walipata alama kuanzia 0 mpaka alama 2, wanafunzi 290,170 (18.78%) walipata alama 4, wanafunzi 226,707 (14.67%) walipata alama 6, na wanafunzi 157,135 (10.17%) walipata alama 8. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa sababu wanafunzi 674, 012 (43.62%) tu walipata alama kuanzia 4 mpaka 8. Pia, wanafunzi 871,137 (56.38%) waliopata alama 0 mpaka 2 hawakufanya vizuri katika upimaji huu. Chati.Na.5 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5.




**Chati Na. 5**: *Ufaulu wa Wanafunzi Katika Swali la 5*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 5 ulikuwa kama ifuatavyo:

Chunguza kwa makini picha ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.




**Maswali**:

(a) Watoto katika picha wanafanya nini?

______________________________________________

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi wa kubaini vitendo vinavyofanywa na watoto kwenye picha. Wanafunzi waliokuwa na ujuzi wa kutosha wa kuchunguza na kutafsiri picha kwa umakini waliandika majibu sahihi ni *kumsaidia mtu asiyeona kuvuka barabara*, *watoto wanaongoza walemavu kuvuka barabara* na *kumsindikiza mzee kuvuka barabara.* Majibu hayo yanaakisi kuwa wanafunzi walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu kujali wengine pamoja na stadi nzuri za kutafsiri picha.

Wanafunzi hawa walielewa kuwa picha inaonesha watoto wawili mvulana na msichana; mmoja akiwa ameshika mkono na mwingine akiwa ameshika fimbo ya mlemavu wa macho wakimsaidia kuvuka barabara kwenye alama ya pundamilia. Hiki kilikuwa ni kitendo kinachoonesha kujali watu wengine. Walijua kwamba vitendo vya kuwajali wengine ni pamoja na kuwaheshimu, kuwapenda, kuwasaidia na kuwalinda kutokana na mambo yanayoweza kuhatarisha usalama wao. Wanafunzi walijua baadhi ya sababu kuu kwa nini ni muhimu kuwajali wengine ni pamoja na: kujenga jumuiya imara zaidi, kukuza uelewano, uwiano wa kijamii, ustawi wa kiakili na kihisia, kupunguza kutengwa, kukuza utamaduni wa ukarimu, utatuzi wa migogoro, kukuza haki ya kijamii, jukumu chanya na kuimarisha ubora wa maisha kwa ujumla.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kusoma na kutafsiri kwa makini matendo yaliyopo kwenye picha. Matokeo yake waliandika majibu au tafsiri isiyo sahihi. Hii pia inaweza kuwa imechangiwa na kuwa na umahiri duni wa kuwajali wengine. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa na wanafunzi yalikuwa: *Wanamlazimisha mtu kuvuka barabara*, *wanakimbia barabarani, watoto wanapigana*, *wanapigwa* na *wanamvuta mzee*. Majibu hayo yanaashiria kuwa wanafunzi walishindwa kuelewa ujumbe wa picha ukiwaonesha mvulana na msichana waliokuwa wamemshika mlemavu wa macho mkono na mwingine akishikilia fimbo wakimvusha upande wa pili wa barabara kwenye kivuko cha pundamilia. Kitendo cha kushika fimbo kilitafsiriwa kuwa ni ishara ya kupigwa, kushikilia mikono kulionekana kumlazimisha mzee kuvuka barabara na kuvuka kwenye alama ya pundamilia ilitafsiriwa vibaya kumaanisha kucheza au kukimbia barabarani.

Sambamba na hilo, wanafunzi wengine walitaja majibu mbalimbali yasiyo sahihi kama; *wanafunzi kukamatwa na mwalimu anayewarudisha shuleni bila sare za shule, wanavuka alama za polisi, wanafuata gari la hatari* na *kuonyesha baba*

*zao njia ya kwenda na kurudi nyumbani.* Kadhalika, wanafunzi wengine waliandika mambo kama vile *kuwapa watoto kazi za nyumbani*, *wanampeleka babu yao kwenye uwanja wa michezo* na *wanampeleka hospitali*. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kwamba watoto waliooneshwa kwenye picha wakimwongoza mtu mwenye ulemavu wa kuona kuvuka barabara walikuwa wakitimiza wajibu wa kijamii wa kusaidia na kuwatunza wazee, na walemavu kuvuka barabara.

(b) Je, tabia inayofanywa na watoto hao ni ya aina gani ?

____________________________________________

Swali hili lilipima uelewa wa wanafunzi wa aina iliyooneshwa na watoto kwenye picha. Wanafunzi waliotafsiri vizuri picha na wale waliokuwa wanafahamu aina ya tabia iliyooneshwa na watoto kwenye picha, waliweza kutoa majibu sahihi kuwa ni *tabia njema* au *tabia sahihi*, *tabia njema ya upole*. Wanafunzi hao walijua kuwa tabia njema ina maana ya matendo na mwenendo unaochukuliwa kuwa ni sawa kimaadili, unaokubalika kijamii na unaofaa kwa mahusiano chanya baina ya watu. Tabia hizi mara nyingi hujengwa na kanuni za kitamaduni na matarajio ya jamii. Viashiria vya tabia njema ni pamoja na uaminifu, heshima, utu wema, huruma, uwajibikaji na ushirikiano. Wanafunzi hawa walielewa kuwa kitendo kilichofanywa na watoto hao cha kumsaidia mtu mwenye ulemavu kuvuka barabara ni kilionesha kujali na kilikuwa ni ishara ya tabia njema.

Kinyume chake, wanafunzi walioshindwa kutafsiri picha na wale ambao hawakujua aina za tabia walitoa majibu yasiyo sahihi. Mfano, walitaja vitu kama *aina mbili za barabara*, *njia za kupita barabara*, *kucheza barabarani*, *kuvuka barabara ya lami*, *fimbo ya mzee inashikiliwa ili kumsaidia kuvuka barabara, ni tabia ya kufanya kazi za ndani na kufua, nguo, watoto wawili*, *wana kugusa fimbo ya babu* na *mazingira ya barabara*. Majibu kama haya yasiyo sahihi yanaakisi uelewa duni wa kutafsiri picha

baada ya kuangalia vitendo na vipengele vilivyooneshwa kwenye picha.

Kadhalika, wanafunzi ambao hawakuweza kutofautisha tabia njema na mbaya, walitafsiri kitendo cha watoto kumsaidia mtu mwenye ulemavu wa macho kuvuka barabara kuwa ni tabia mbaya. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika mambo kama vile *tabia mbaya*, *ni tabia mbaya kutembea barabarani*, *si jambo zuri kumvuta babu*, *ishara mbaya katika maadili* na *watoto kumfanyia babu vibaya*. Walishindwa kuelewa kwamba kuwasaidia wazee, watu wenye ulemavu, watoto na wagonjwa ni miongoni mwa vitendo vinavyoonyesha tabia nzuri katika jamii. Kiuhalisia, kusaidia makundi hayo ni wajibu ambao kila mmoja anatakiwa kutekeleza katika jamii.

(c) Taja jina la alama zilizochorwa eneo la barabara watoto wanapovukia.

_______________________________________________

Kipengele hiki kilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu alama mbalimbali za barabarani hususani alama milia. Wanafunzi waliofaulu vizuri, walielewa kuwa kivuko cha pundamilia ni njia ya wapita kwa miguu kwenye barabara, ambayo kwa kawaida huwa na mistari myeusi na myeupe inayopishana na inayofanana na ngozi ya pundamilia. Zaidi ya hayo, walikuwa na ufahamu kuwa madhumuni ya kivuko cha pundamilia ni kutoa eneo maalumu na salama kwa waenda kwa miguu kuvuka barabara. Kivuko cha pundamilia ni muhimu sana kwa watumiaji wa barabara kwa namna kadhaa kama vile: usalama wa watembea kwa miguu, muonekano, udhibiti wa magari, wajibu wa kisheria, kipaumbele kwa watembea kwa miguu na ufikikaji.

Kwa upande mwingine, kulikuwa na wanafunzi ambao walishindwa kutoa jibu sahihi. Hali hii ilichochewa na ujuzi duni

kuhusu alama za barabarani au kutoweza kufasiri picha iliyotolewa. Kwa hivyo, walijibu swali hili kwa kutoa majibu yasiyo sahihi kama vile *Kwenye reli ya rangi nyeupe,kwenye njia za reli* na *juu ya reli*. Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kwamba vipande vipana vyeusi na vyeupe vilivyochorwa kwenye barabara ambapo watoto walikuwa wakivuka ni kivuko cha alama milia na si reli. Pia, wangeweza kujua kwamba kivuko cha pundamilia kinakuza usalama wa watembea kwa miguu, kudhibiti magari na kuunda mazingira yaliyopangwa na salama zaidi kwa watumiaji wote wa barabara.

Majibu mengine yasiyo sahihi yalijidhihirisha wanafunzi kutaja bila mpangilio chochote walichokiona kwenye picha. Baadhi ya wanafunzi kwa mfano, waliandika yafuatayo: *taa za barabarani*, *gari*, *shina*, *nyumba*, *mti na watu*, *nyumba nzuri*, *gari la kupita*, *barabara nzuri* na *duka zuri*, *gari linapita mahali watoto wanavuka barabara*, *duka*; *ni alama ya duka* na *barabara*, *ishara ya taa ya trafiki* na *rangi nyeusi na nyeupe*. Wengine, walitaja *kamera ya ulinzi kwa wagonjwa* na *magari, kwenye kituo cha mabasi*, *majengo*, *waya wa umeme*, *lami* na *barabara kuu*. Haya yote yanaonesha kukosekana kwa umahiri wa kutafsiri picha kwa wanafunzi.


Vilevile, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kuelewa swali waliishia kuchambua rangi na kazi za taa za barabarani zilizooneshwa kwenye picha kando ya barabara karibu na Kivuko cha alamamilia. Baadhi ya wanafunzi, kwa mfano, walieleza: *kijani na nyekundu, rangi ya kijani inaruhusu watu kuvuka*, *kwenda kwakijani, kijani na nyekundu kwenye alama ya trafiki, nyekundu na kijani kuruhusu na hairuhusu kuvuka zikiwa zinawaka*.

(d) Je, ni kwanini watoto wanavuka barabara sehemu yenye alama iliyotajwa katika (c) ?

________________________________________

Swali katika kipengele hiki llilipima uelewa wa wanafunzi wa matumizi ya alama ya pundamilia na umuhimu wake kwa watumiaji wa barabara. Wanafunzi ambao walikuwa na ufahamu wa matumizi mbalimbali ya alama za barabarani waliandika majibu sahihi ambayo ni pamoja na, *ni sehemu sahihi ya kuvuka barabara, ni sehemu salama kwa watembea kwa miguu kufika ng'ambo ya pili*, *kwa sababu alama za pundamilia huchorwa hapo na kuwaruhusu kuvuka barabara* na *kwa sababu ya uwepo wa alama za barabarani zinazowaruhusu kuvuka barabara.* Majibu hayo mazuri yanaonesha kuwa wanafunzi walielewa vyema matumizi ya alama za barabarani hasa aina ya *pundamilia*.

Zaidi ya hayo, walikuwa na ufahamu kuhusu umuhimu wa kuvuka sehemu yenye alama milia ambapo huongeza usalama wa watembea kwa miguu, husaidia kudhibiti mtiririko wa watembea kwa miguu na magari, hupunguza hatari ya ajali na watembea kwa miguu wana haki ya kuvuka barabara na madereva wanatarajiwa kuwaruhusu waenda kwa miguu wavuke barabara. Kielelezo Na 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya wanafunzi kwa swali la 5.



**Maswali**

(a) Watoto katika picha wanafanya nini?

Wanavuka barabara

(b) Je, tabia inayofanywa na watoto hao ni ya aina gani?

nzuri

(c) Taja jina la alama zilizochorwa eneo la barabara watoto wanapovukia.

pundamilia

(d) Je, ni kwanini watoto wanavuka barabara sehemu yenye alama iliyotajwa katika (c)?

kwasababu kuna Kivuko cha barabara

Kwasababu nikivuko cha barabara


**Kielelezo Na.3.1**: *Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi Katika Swali la 5*

Kinyume chake, wanafunzi wasio na ufahamu wa kutosha kuhusu matumizi ya alama mbalimbali za barabarani waliandika majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, *kwa watoto kuvuka, kwa watoto kurudi, tabia mbaya, mahali ambapo kuna mtu anayewaangalia kutoka nyuma yao, kwa sababu hawakujua uwepo wa zebra crossing na walikuwa na hakuna taarifa yoyote*. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hawakuelewa swali. Pia, hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya umuhimu wa kivuko cha alamamilia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi hawakufahamu kuwa katika kivuko cha *alamamilia* ni eneo salama kwa watembea kwa miguu kuvuka barabara. Hivyo, waliishia kuwalaumu watoto waliokuwa wakimsaidia mtu kuvuka barabara kwa kutumia alama hizo. Baadhi ya wanafunzi kwa mfano waliandika: *gari litawagonga, mahali pa hatari*

*ambapo gari na pikipiki hupita, ilikuwa ishara ya hatari kwa sababu gari lilikuwa linakuja na kwa bahati nzuri lilisimama kuwaruhusu kuondoka barabarani, walikuwa wakivuka na walikuwa wakorofi hawana nidhamu, wanasimamisha magari na Ni jambo baya kupita katikati ya barabara*. Walitakiwa kuelewa kwamba vivuko vya *alamamilia* vimewekwa mahali ambapo ni salama kwa watoto na watu wengine kuvuka barabara. Vilevile, alama ya pundamilia inaonya/kutahadharisha madereva kuchukua tahadhari kuwa kunaweza kuwa na watembea kwa miguu wanaovuka au wanaosubiri kuvuka barabara. Kwa maneno mengine, inawaambia madereva kuwaruhusu watembea kwa miguu kwenye kivuko.

Aidha, wanafunzi wengine walipuuza umuhimu wa kutumia vivuko vya pundamilia wakati wote wanapotaka kuvuka barabara. Badala yake, waliandika majibu yanayoonesha kuwa vinapaswa kutumika shuleni, vituo vya mabasi tu au mtu anapokuwa na haraka. Baadhi ya majibu yaliyotolewa na wanafunzi hao yalikuwa kama ifuatavyo: *Kwa sababu ni barabara inayotumika kwa watu wanaokwenda kupanda basi, kwa sababu wanapita karibu na shule, walikuwa na haraka, wana mgonjwa na kwa sababu watu wa mjini wanasimama hapo*. Majibu kama haya yanazidisha dhana kwamba wanafunzi hawa walijenga hoja zao kwa kuegemea sehemu ambazo kivuko cha pundamilia hupatikana hasa sehemu zenye watu wengi kama vile kwenye stendi za mabasi, sokoni na maeneo ya shule. Mbali na hilo, walishindwa kuelewa kuwa matumizi ya njia ya pundamilia lazima izingatiwe na watumiaji wote wa barabara kwa sababu inasaidia kupunguza ajali za barabarani kwa watumiaji wa barabara, inatilia mkazo wazo la kuwa baadhi ya maeneo ni maalumu kwa ajili ya vivuko vya waenda kwa miguu, na kila mtu afuate sheria kwa ajili ya kujenga mazingira salama ya barabara. Muonekano wa alama ya pundamilia husaidia madereva kupunguza kasi na kusimama ikiwa ni lazima. Kielelezo Na 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya wanafunzi kwa swali la 5.



**Maswali**

(a) Watoto katika picha wanafanya nini?

Kazi nzuri sanakabisa kufagia uchafu wote sana

(b) Je, tabia inayofanywa na watoto hao ni ya aina gani?

kutoroka shuleni bila kuachiwa

(c) Taja jina la alama zilizochorwa eneo la barabara watoto wanapovukia.

rami na barabara alama za rami zeupe

(d) Je, ni kwanini watoto wanavuka barabara sehemu yenye alama iliyotajwa katika (c)?

rami wanaizula kwa jili gali lipite
wanakati ili waka Pande gali


**Kielelezo Na. 3.2**: *Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi Katika Swali la 5*

## 2.6 Swali la 6: Kudumisha Amani

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani* na umahiri mahususi wa *Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine*. Swali hili lilipima ujuzi wa wanafunzi wa kusoma kwa makini kifungu cha habari na kisha kuandika majibu katika nafasi zilizoachwa wazi katika kila vipengele (a) mpaka (d). Kifungu cha habari kilihusu uhusiano mwema baina ya nchi ya Tanzania na mataifa mengine ya Afrika.

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa kama ifuatavyo: Wanafunzi 794,547 (51.42%) walipata ufaulu wa alama 0 hadi 2, wanafunzi 324,346 (20.99%) walipata alama 4, wanafunzi 269,074 (17.41%) walipata alama 6 na wanafunzi 157,182 (10.17%) walipata alama 8. Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa kiwango cha wastani kwa kuwa wanafunzi 750,602 (48.58%) walipata alama kuanzia 4 hadi 8. Wanafunzi

wengine 794,547 (51.42%) hawakufanya vizuri kwa kuwa walipata alama kuanzia 0 hadi alama 2. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 6.




**Chati Na. 6**: *Ufaulu wa Wanafunzi Katika Swali la 6*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 6 ulifanyika kama ifuatavyo:

Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu vipengele (a) – (d) katika sehemu zilizoachwa wazi.

*Nchi ya Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye mahusiano mazuri na mataifa mengine ya Afrika. Mahusiano hayo yanatokana na Tanzania kujitolea kusaidia katika ukombozi wa mataifa mengine ya Afrika yaliyokuwa yakitawaliwa. Baadhi ya mataifa yaliyohusika na harakati za ukombozi ni pamoja na Msumbiji, Angola na Afrika Kusini. Pia Tanzania imeshiriki kutatua migogoro ya mataifa mengine kama Rwanda, Burundi na Kenya. Migogoro katika nchi husababisha wananchi wa nchi husika kukimbilia nchi za jirani na kuwa wakimbizi. Tanzania imekuwa ikiwahifadhi wakimbizi toka nchi za jirani zenye*

*machafuko ya kisiasa kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda, Burundi, Somalia na Sudani. Wakimbizi hao huhifadhiwa kwenye kambi zilizopo mikoa ya Kigoma, Kagera na Katavi. Katika Bara la Afrika, Tanzania ni mfano halisi kwa jinsi inavyohusiana vizuri na nchi nyingine*.

**Maswali**:

(a) Taja nchi mbili zilizosaidiwa na Tanzania kupata uhuru wake.

(i) ___________________________________________

(ii) ___________________________________________

Swali hili lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya mchango wa nchi ya Tanzania katika kupata uhuru kwa baadhi ya nchi za Afrika. Wanafunzi waliosoma kwa makini na kuelewa kifungu walikuwa na uwezo wa kutambua nchi hizo kwa usahihi kuwa ni *Msumbiji* na *Angola*. Majibu haya yanathibitisha umahiri wa wanafunzi katika kutambua masuala ya uhusiano wa kimataifa. Wanafunzi walitambua kuwa Tanzania ilijitoa kama ngome ya nchi na makundi yanayopigania ukombozi kwa kuwa mwenyeji wa vikosi vya vuguvugu nyingi kwa mfano, African National Congress (ANC) na Pan African Congress (PAC) kutoka Afrika Kusini, Mozambique Liberation Front (FRELIMO). Vuguvugu la Watu wa Ukombozi wa Angola (MPLA) na Umoja wa Kitaifa wa Afrika wa Zimbabwe (ZANU).Wengine walikuwa Zimbabwean African Peoples' Union (ZAPU) na South West African People's Organization (SWAPO) kutoka Namibia. Wanafunzi hawa pia walifahamu kuwa Tanzania ilipokea na kuwahifadhi wakimbizi kutoka katika mapambano katika nchi za kusini mwa Afrika. Mbali na hayo, yalikuwa ni makao makuu ya iliyokuwa kamati ya Umoja wa Afrika yaani African Liberation Committee, ambayo ilijikita tu katika harakati za ukombozi wa nchi za Kiafrika zilizokuwa chini ya himaya ya wakoloni.

Vilevile, wanafunzi wasio na ujuzi wa kutosha wa ufahamu walitaja majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walitaja mataifa ambayo hayakusaidiwa na Tanzania katika harakati zao za kupigania uhuru kama vile *Burundi, Rwanda*, *Malawi* na *Kenya*. Majibu haya pengine yalichangiwa na Tanzania kuhusika katika utatuzi wa migogoro katika nchi zilizotajwa na hivyo wanafunzi hao walichanganya mambo.

Aidha, wanafunzi wengine walitaja sehemu za Muungano wa Tanzania kwa kueleza mambo kama vile *Zanzibar* na *Tanganyika*. Hawa walipaswa kuelewa kwamba Zanzibar na Tanganyika ni nchi huru, zilizoungana mwaka 1964 na kuunda Tanzania kwa hiyo, yalikuwa majibu yasiyo sahihi kwa mujibu wa swali. Zaidi ya hayo, baadhi ya wanafunzi walifasili swali hilo kumaanisha nia ya Tanzania kushiriki katika harakati za kupigania uhuru wa nchi nyingine. Mambo haya yaliyotajwa kama vile *iliamua kujitolea yenyewe na ilitoa tu msaada kwa nchi.*

Zaidi ya hayo, baadhi ya wanafunzi walitaja tunu za taifa kama vile *uzalendo* na *utu*. Aidha, uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unadhihirisha kuwa kuna wanafunzi ambao walishindwa kuelewa swali na hivyo walitaja majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu swali hili kwa kutaja rangi na masuala mengine yasiyohusiana kama vile *bluu, nyeusi*, na *yale ya mikoa* na *timu za michezo*. Mwanafunzi mwingine alitaja mambo yanayohusiana na rasilimali zinazopatikana Tanzania kama vile *maji, misitu* na *madini*.

Hali kadhalika, mwanafunzi mwingine alieleza miaka ambayo Tanzania ilipata uhuru wake kutoka kwa wakoloni wa Uingereza pamoja na mwaka ambao Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kuunda Tanzania kwa kutaja miaka *1961* na *1964.*

Kulikuwa na wanafunzi ambao walifasili vibaya swali na kuandika *sababu za* utitiri wa wakimbizi nchini Tanzania. Walitaja mambo kama vile *vurugu za kisiasa nchini Rwanda* na *Burundi* na *kwa sababu Kongo inapigana wenyewe kwa wenyewe*. Hii inaonesha kwamba wanafunzi hao walishindwa kuelewa swali.

(b) Taja nchi mbili zenye migogoro katika habari uliyoisoma.

(i) ________________________________________

(ii) ________________________________________

Swali hili liliwataka wanafunzi kutaja nchi mbili ambazo zimekuwa na migogoro katika bara la Afrika kwa kurejelea kifungu walichosoma. Wanafunzi waliosoma kifungu kwa makini na kukielewa, waliweza kutambua nchi zenye migogoro. Nchi zilizotajwa ni kama vile *Burundi, Rwanda* na *Kenya*. Uchaguzi wa jibu sahihi unaonesha uelewa wa wanafunzi kuhusu dhana ya migogoro. Dhana hiyo ina maana kutoelewana kwa muda mrefu au vurugu kati ya makundi au mataifa tofauti. Aidha, walielewa nchi nyingine barani Afrika ambazo zinakabiliwa na migogoro au zinakabiliwa na changamoto zinazoendelea za usalama. Baadhi ya nchi hizo ni pamoja na: *Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Somalia, Nigeria, Libya* na *Mali*. Katika nchi hizo, migogoro ilitokana na mambo mbalimbali kwa mfano, *uchaguzi* na *migawanyiko mirefu ya kikabila*.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi ambao hawakuelewa vyema kifungu hicho walipotoka kwa kutaja nchi jirani na Tanzania ambazo hazikuakisiwa popote katika kifungu hicho. Kwa mfano, walitaja nchi kama *Malawi, Zambia* na *Uganda*. Majibu hayo yanakiuka matakwa ya swali kwani wanafunzi walipaswa kulijibu kwa kurejelea kifungu walichosoma.

Wanafunzi wengine ambao hawakuelewa lengo la swali waliandika hoja kama *nchi zote, mataifa mengine ya Afrika* na *bara la Afrika*. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kwamba mchango wa Tanzania katika mapambano ya ukombozi ulijikita katika baadhi ya nchi hasa zile za Kusini mwa Afrika kwa mfano Msumbiji, Afrika Kusini, Zimbabwe na Angola. Vilevile, baadhi ya wanafunzi walielezea aina na sababu za kuibuka kwa wakimbizi katika sehemu mbalimbali za dunia. Walitaja mambo hayo kuwa ni *migogoro ya kikabila, kutokuwa na mahusiano mazuri, ukosefu wa demokrasia, vita* na *vifo na migogoro kati ya wakulima na wafugaji*.

Vilevile, wengine walitoa hoja zinazohusiana na athari za vita vya wenyewe kwa wenyewe. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alieleza: *inawalazimisha raia wa nchi hiyo kuziacha nchi zao kwenda nchi nyingine*. Zaidi ya hayo, baadhi ya wanafunzi walieleza hatua zilizochukuliwa na Tanzania kushughulikia wakimbizi ambapo wengine walieleza juu ya athari mbalimbali za wakimbizi kwa nchi zinazowahifadhi. Baadhi ya majibu yaliyotolewa na wanafunzi hawa yalikuwa kwa mfano*, Tanzania inawapokea watu hao na kuwaweka kambi, wanachafua mazingira, na ni watu hatari na vyanzo vya maji na kukata miti*.

Mwishowe, baadhi ya wanafunzi waliandika hoja zisizo na umuhimu na kuziwasilisha kama majibu ya kipengele hiki. Baadhi ya majibu hayo yalikuwa kama, *Tanzania, Zanzibar, Tanganyika, Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo, ni nchi ya SADC na ukombozi wa Afrika.*

(c) Watu wanaokimbia nchi yao kwa sababu ya migogoro huitwaje?

________________________________________________

Swali lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu dhana ya Wakimbizi kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha habari. Wanafunzi walioelewa kifungu hicho waliandika jibu sahihi *Wakimbizi*. Wanafunzi hao walijua kwamba wakimbizi ni watu ambao wamelazimika kuondoka katika nchi zao kutokana na sababu mbalimbali kama vile mateso, vita, vurugu, majanga ya asili au ukiukaji wa haki za binadamu. Wanatafuta kimbilio katika nchi nyingine kwa matumaini ya kupata ulinzi na usalama. Walikuwa na ufahamu kuhusu mambo kadhaa yanayochangia kuwepo kwa wakimbizi katika Bara la Afrika ikiwa ni pamoja na migogoro na vita, ukosefu wa utulivu wa kisiasa, majanga ya asili, mateso na ubaguzi, matatizo ya kiuchumi na mambo ya mazingira.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu kujenga urafiki na mataifa mengine, walishindwa kuandika majibu yaliyo sahihi. Kwa mfano, badala ya kutaja jina la watu waliokimbia nchi yao baadhi ya wanafunzi walitaja majina ya nchi mbalimbali zinazopatikana barani Afrika. Baadhi ya nchi zilizotajwa na wanafunzi ni kwa mfano, *nchi ya Tanzania, Msumbiji, Kongo, Zambia, Burundi* na *Somalia*.

Vilevile, wanafunzi wengine walitaja majina ya mikoa na wilaya nchini Tanzania ambako kambi za wakimbizi zinapatikana. Kwa mfano, walitaja Kagera, Katavi na Kigoma. Pia, baadhi ya wanafunzi walishindwa kutofautisha watu wanaohama kutoka nchi zao kwa mapenzi yao kwenda nchi nyingine na wakimbizi. Kwa hiyo, waliandika majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika mambo yafuatayo: *Wahamiaji ni watu wanaotoroka kutoka mataifa makubwa.* Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kwamba wahamiaji ni watu ambao kwa hiari yao wanahamia maeneo mengine au nchi za kigeni kwa kudumu au kwa muda kutafuta kazi au hali bora ya maisha. Walipaswa kutambua kwamba wakimbizi ni watu

wanaolazimika kuhamia nchi nyingine kutafuta maeneo salama kwa ajili ya kuokoa maisha Ayao kufuatia machafuko katika nchi zao.

Majibu ya baadhi ya wanafunzi yaliakisi mtazamo na fikra hasi za wanafunzi kwa wakimbizi. Baadhi yao walitaja *kitendo cha kuhamia nchi ya kigeni kama ishara ya kutokuwa na aibu na usaliti kwa nchi zao.* Wengine walitoa hoja kama: *wao ni waoga na si wazalendo, watu wa kabila, wagonjwa, watumwa na watu wanaokimbia nchi zao ni wajinga*. Aidha, wanafunzi wengine walienda mbali na kuelezea tabia za baadhi ya wakimbizi kwa kuwataja wahusika kama: *wahalifu, hatari kwa ng'ombe, wengine ni majambazi, wanavamia watu kijijini na si watu wema. Majibu kama haya yaliathiriwa na uzoefu wa baadhi ya wanafunzi katika maeneo ambayo wakimbizi wanahifadhiwa*. Ni ukweli kuwa baadhi ya maeneo hayo yana matukio mbalimbali ya uhalifu na changamoto za uhifadhi wa mazingira.


(d) Kwa nini Tanzania ina mahusiano mazuri na mataifa mengine ya Afrika?

__________________________________________

Swali hili liliwataka wanafunzi kubainisha mambo yanayochangia uhusiano chanya wa Tanzania na Mataifa Mengine. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa kulikuwa na wanafunzi walioelewa vizuri kifungu na kutoa sababu sahihi za uhusiano mzuri. Baadhi ya sababu husika zilikuwa kama zifuatazo: *Kwa sababu Tanzania inashiriki katika utatuzi wa migogoro ya nchi nyingine za Afrika na Kwa sababu Tanzania imesaidia nchi nyingine katika mapambano yao ya ukombozi*. Majibu kama haya yanathibitisha kwamba wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu jinsi Watanzania walivyojitolea maisha na mali zao katika kusaidia ukombozi wa baadhi ya nchi za Afrika kutoka mikononi mwa wakoloni.

Sababu nyingine kuu za uhusiano huo mzuri ni pamoja na sera ya kigeni isiyofungamana na upande wowote, kuishi pamoja kwa amani, ushirikiano wa kiuchumi, kuwa mwanachama wa mashirika mbalimbali ya kimataifa, ushirikiano wa kimaendeleo, uhusiano wa kitamaduni na watu na watu na michango ya kibinadamu.

Sababu nyingine zinazofanya Tanzania kuwa na uhusiano mzuri na mataifa mengine ni kama vile: Tanzania inashirikiana na mataifa mengine katika matumizi ya miundombinu yake kama vile reli, bandari na barabara, kuwa na muunganiko wa watu kutoka ndani na nje ya nchi yetu wanaovutiwa na kuwepo kwa maliasili kama madini, rasilimali ardhi, mbuga za wanyama na hifadhi za taifa kuja kuwekeza au kufanya ziara za kitalii nchini Tanzania. Kielelezo Na 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi ambaye alijibu kwa usahihi swali la 6.



**Maswali**

(a) Taja nchi mbili zilizosaidiwa na Tanzania kupata uhuru wake.

(i) Msumbiji

(ii) Angola.

(b) Taja nchi mbili zenye migogoro katika habari uliyoisoma.

(i) Rwanda

(ii) Burundi

(c) Watu wanaokimbia nchi yao kwa sababu ya migogoro huitwaje?

Wakimbizi

(d) Kwa nini Tanzania ina mahusiano mazuri na mataifa mengine ya Afrika?

Mahusiano hayo yanatokana na Tanzania kujitolea kusaidia. Katika [illegible] ya mataifa mengine ya Afrika yaliyokuwa yakitawaliwa.

**Kielelezo Na. 4.1**: *Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 6*


Kwa upande mwingine, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulionyesha kuwa wanafunzi waliojibu swali hili kimakosa walikosa ujuzi wa kutosha wa ufahamu. Kwa hiyo, walitoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu kama; *kwa sababu maalumu nchi za Ulaya zinakinzana na Tanzania, kwa sababu Tanzania ilipata uhuru kwa msaada wa Julius Nyerere*, *Tanzania ni chanzo cha mahusiano hayo na kutoroka nchi zao kuja Tanzania*. Majibu hayo yanaonesha kuwa, wanafunzi hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu kudumisha uhusiano mzuri na mataifa mengine. Wanafunzi hao walitarajiwa kufahamu kuwa Tanzania ina uhusiano mzuri na nchi nyingine za Afrika kwa sababu ya umuhimu wake kihistoria katika harakati za kupigania uhuru.

Zaidi ya hayo, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi wengi hawakujua nafasi ya Tanzania katika harakati za ukombozi wa baadhi ya nchi za Kiafrika, walieleza sababu zinazopingana na nia njema ya Tanzania ya kusaidia harakati za mapambano. Majibu ya namna hii yalikuwa kama *kwa sababu Tanzania iko karibu na nchi hizi, kwa sababu ina uhuru wake, ikikwepa wakimbizi*, *Tanzania ni mfano wa nchi zenye uhusiano mzuri na nchi nyingine* na *kwa sababu zinaiba watu*. Pia, waliongeza, waliongeza kutaja maneno mengine kama: *kwa sababu ni uhusiano wa kusaidiana kutatua migogoro ya Tanzania*, *kwa sababu Tanzania ni huru na ya kidemokrasia, kwa sababu ya fursa ya kibiashara kwa sababu Tanzania ni mfano mzuri wa kijeshi wa Afrika, kwa sababu ya migogoro na manufaa kwa yenyewe na kwa sababu ya kisiasa.*

Wanafunzi hawa walitarajiwa kuelewa kwamba ushiriki wa Tanzania katika harakati za ukombozi wa baadhi ya nchi za Kiafrika haukuwa wa bahati mbaya au wenye nia nyingine za siri. Ushiriki wake katika harakati hizo ulichochewa na nia ya utekelezaji wa sera yake ya mambo ya nje, ambayo imejikita katika misingi ya: ulinzi wa uhuru, haki, haki za binadamu, usawa na demokrasia na kukuza ujirani mwema. Misingi

mingine ni pamoja na kukuza umoja wa Afrika na kuunga mkono Umoja wa Mataifa katika kutafuta maendeleo ya kiuchumi ya kimataifa, amani na usalama.

Zaidi ya hayo, kulikuwa na wanafunzi waliokosa; ufahamu, matokeo yake, walishindwa kuelewa mahitaji ya swali. Kutokana na udhaifu huo, walijadili masuala yasiyo na umuhimu kuhusiana na utajiri wa asili wa Tanzania. Mambo hayo yaliyotajwa ni kama vile *samaki, wanyama pori, kwa sababu ya madini, mbuga za wanyama, kwa sababu ya kuwa na chakula kingi na ardhi nzuri na watanzania ni wema*. Walishindwa kutambua kuwa utajiri wa asili sio sababu za uhusiano mzuri kati ya Tanzania na nchi nyingine bali ni mambo yanayowavutia watu kutembelea na kuwekeza Tanzania. Mbali na hilo, wanafunzi wengine waliandika majibu yasiyolingana ama kuhusiana na mahitaji ya swali lililoulizwa. Kwa mfano waliandika: *Bara la Afrika, kwa sababu Tanzania ilitawaliwa na wakoloni, watu wengine waliosuluhisha migogoro ni Nyerere nchini Tanzania na kuhamia Tanzania nchi za mbali.* Yamkini, hii ilitokana na kutoweza kwa wanafunzi kuelewa kifungu cha habari. Kielelezo Na 4.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mwanafunzi katika swali la 6.



**Maswali**

(a) Taja nchi mbili zilizosaidiwa na Tanzania kupata uhuru wake.

(i) Mutogoto

(ii) migogoro

(b) Taja nchi mbili zenye migogoro katika habari uliyoisoma.

(i) Shule na Migogoro

(ii) Shinyanga na geitA

(c) Watu wanaokimbia nchi yao kwa sababu ya migogoro huitwaje?

diniani

(d) Kwa nini Tanzania ina mahusiano mazuri na mataifa mengine ya Afrika?

Kufanya usafi

Shule

***Kielelezo Na. 4.2***: *Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 6*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Uchambuzi wa kila umahiri katika somo la Uraia na Maadili unaonesha kuwa kati ya aina tano (5) za umahiri uliopimwa, wanafunzi walifanya vizuri kwenye umahiri wa *Kuwa mwadilifu* uliopimwa kwenye swali la 1 (81.71%), *Kuwa mwajibikaji* uliopimwa kwenye swali la 4 (74.27%) na *Kuithamini jamii* uliopimwa kwenye swali la 3 (69.35%). Wanafunzi wengine walipata ufaulu wa wastani katika umahiri wa Kudumisha amani uliopimwa katika swali la 6 (48,58%) na umahiri wa Kuithamini jamii katika swali la 5 (43.62%) na umahiri wa kuheshimu jamii uliopimwa katika swali la 2 (20.31%) ulikuwa na ufaulu hafifu.

Aidha, ulinganifu wa ufaulu wa umahiri kati ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne kwa mwaka 2023 na 2022 unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu cha umahiri wa *Kuwa mwadilifu* umeongezeka kutoka ufaulu hafifu (31.33%) katika mwaka 2022

hadi ufaulu mzuri (81.71%) katika mwaka 2023. Ufaulu katika umahiri wa *Kuwa mwajibikaji* umeendelea kuwa wa kiwango kizuri (74.27%) katika mwaka 2023 ikilinganishwa na (68.25%) katika mwaka 2022.

Pia, ufaulu wa *Kuithamini jamii* umeendelea kuwa na kiwango cha wastani (56.49%) katika mwaka 2023 ikilinganishwa na (56.60%) katika mwaka 2022. Vilevile, ufaulu wa umahiri wa *Kudumisha amani* umeendelea kuwa wa wastani (48.58%) katika mwaka 2023 ikilinganishwa na (52.89%) katika mwaka 2022. Umahiri wa *Kuwa mstahimilivu* ulikuwa na ufaulu wa wastani (55.27%) katika mwaka 2022. Hata hivyo, mwaka 2023 haukupimwa. Mwisho, katika umahiri wa *Kuheshimu jamii,* ufaulu ulishuka kutoka katika kiwango cha wastani (61.68%) katika mwaka 2022 na kuwa wa kiwango hafifu (20.31%) katika mwaka 2023.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili 2023 umeonesha kuwa kwa ujumla wanafunzi wamefaulu kwa kiwango kizuri. Wanafunzi waliopata Daraja A hadi D walikuwa asilimia 85.52. Aidha, wanafunzi wachache ambao ni asilimia 14.48 wamepata kiwango hafifu cha ufaulu wa Daraja E. Wanafunzi waliofanya vizuri katika upimaji huu walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika aina za umahiri uliyopimwa. Aidha, wanafunzi hao waliweza kubaini matakwa ya maswali. Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi umebaini changamoto mbalimbali walizokuwa nazo wanafunzi na hivyo kuwa na ufaulu hafifu. Baadhi ya changamoto hizo ni kutokuwa na maarifa ya kutosha katika aina za umahiri uliopimwa, kushindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo, kushindwa kuandika majibu yanayoeleweka. Vilevile, wanafunzi walionesha ukosefu wa

umahiri katika maswali ya stadi za kutafsiri picha, na kifungu cha habari katika swali la 5 na 6 mtawalia.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Uraia na Maadili hususan katika umahiri wa Kuheshimu jamii, Kuithamini jamii na Kudumisha amani yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa:

(a) Walimu wa somo waendelee kubuni na kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea wanafunzi umahiri unaokusudiwa. Baadhi ya mbinu hizo ni pamoja na:

(i) Igizo dhima, kujifunza kwa kuuliza na ujifunzaji wa ushirikiano; mbinu ambazo hujumuisha matendo kama: kufikiri na kushirikiana, majadiliano katika makundi madogo au wawili. Hii itasaidia kuboresha Maarifa ya kijamii na uwezo wa mwanafunzi kufikiri vizuri.

(ii) Kutumia mbinu ya kutembelea maeneo mbalimbali ambayo wanafunzi wanaweza kujifunza umahiri mbalimbali wa somo. Mbinu hii ni muhimu kwa kufundisha umahiri wa kudumisha amani, kwa kuwa unahusisha kutembelea mazingira maalumu ya kujifunza na kusikia taarifa za moja kwa moja kutoka kwa wahusika au wataalamu wa eneo hilo.

(b) Wanafunzi wafundishwe kwa kina na kupewa mbinu nyingi zinazohusiana na maswali ya kuangalia picha kwa umakini na kusoma ufahamu kisha kujibu maswali kwani kwa mujibu wa uchambuzi wa majibu ya wanafunzi, maswali ya aina hiyo yanaonekana kuwapa changamoto.

(c) Wanafunzi wapewe shughuli nyingi za upimaji wa umahiri darasani kama vile mazoezi, majaribio na mitihani ili kukuza na kuboresha uwezo wao wa kujibu maswali.

(d) Walimu kwa kushirikiana na wazazi wabuni mbinu za kuwawezesha wanafunzi kupenda kujisomea vitabu vya kiada na ziada ili kuimarisha uelewa wa umahiri wa somo la Uraia na Maadili kwa ujumla.

(e) Walimu wanapaswa kujua uwezo na udhaifu wa mwanafunzi na kurekebisha mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji kwa ajili ya kuboresha.

***Kiambatisho***

Ulinganifu wa ufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022

| **Na.** | **Umahiri** | **Upimaji 2023** | | | | **Upimaji 2022** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Ufaulu wa kila swali** | | | | **Ufaulu wa kila swali** | | | |
| | | **Namba ya swali** | **faulu katika kila swali (%)** | **Wastani wa ufaulu katika umahiri (%)** | **Maoni** | **Namba ya swali** | **Ufaulu katika kila swali(%)** | **Wastani wa Ufaulu katika umahiri (%)** | **Maoni** |
| 1 | Kuwa Mwajibikaji | 4 | 74.2.7 | 74.2.7 | Vizuri | 1 | 68.25 | 68.25 | Vizuri |
| 2 | Kuheshimu Jamii | 2 | 20.31 | 20.31 | Hafifu | 2 | 61.68 | 61.68 | Wastani |
| 3 | Kuwa Mstahimilivu | | | | | 3 | 56.60 | 56.60 | Wastani |
| | Kuithamini Jamii | 3 | 69.35 | 69.35 | Vizuri | - | - | - | - |
| 4 | Kuithamini Jamii | 5 | 43.62 | 43.62 | Wastani | 4 | 55.27 | 55.27 | Wastani |
| 5 | Kuwa Mwadilifu | 1 | 81.71 | 81.71 | Vizuri | 5 | 52.89 | 52.89 | Wastani |
| 6 | Kudumisha Amani | 6 | 48.58 | 48.58 | Wastani | 6 | 31.33 | 31.33 | Hafifu |